# Nipashe

Alhamisi Februari 6, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581944

epaper.ippmedia.com / www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com


**KAMATI** ya Bunge yapigwa na butwaa ongezeko matumizi dawa za kulevya za kemikali nchini

UKURASA 3



UKURASA 8

**RIPOTI MAALUM -2**
Wataalamu watoa angalizo serikalini wananchi kutozwa huduma ya choo



**MAPIGANO DRC...**
Matumaini mapya mkutano wa SADC, EAC Dar es Salaam

UKURASA 19

MIAKA 48

# CCM yashtuka

**MWENYEKITI** Samia aelekeza njia kuwavuta vijana, wasifu wa wagombea wawekwa hadharani... Endelea Ukurasa wa 2



Mgombea urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Samia Suluhu Hassan akiwa na mgombea mwenza, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi pamoja na mgombea urais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (gari la nyuma), wakiwapungia mikono wanachama na wananchi, baada ya kutambulishwa katika Maadhimisho ya Miaka 48 ya Kuzaliwa kwa CCM kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 17

## MADAI WATOTO KUJITEKA YAIBUA WATAALAMU

TUKIO la watoto wa miaka 16 na 12 kudaiwa kujiteka ili kujipatia fedha, limewaamsha wataalamu wa afya na kuwashauri wazaz...



UKURASA WA 24

## MO: KIBU HAUZWI, SIMBA IKIWAANDALIA DOZI FOUNTAIN GATE

IKITARAJIWA kuwakabili wenyeji Fountain Gate FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara...



## Nyama ya nguruwe isiyoiva yatajwa maficho ya kifafa

UKURASA 18

## USAID yafunga akaunti zake, waandamana kumpinga Trump

UKURASA 2

MICHEZO YANGA YAMKARIBISHA HAMDI KIBABE UK. 24 KATUNI UK. 6

# USAID yafunga akaunti zake, waandamana kumpinga Trump

**Na Elizabeth Zaya**

WAKATI joto likiendelea kupanda la kusitishwa kwa miradi ya afya, Shirika la Misaada ya Kimataifa (USAID), limejiondoa kwenye mitandao ya kijamii na kufunga tovuti yake, huku wafuasi wa Chama cha Demokratiki wakifanya maandamano na kupinga uamuzi wa Rais wa Marekani, Donald Trump kusimamisha shughuli zake kwa siku 90.

Aidha, kumekuwa na maoni tofauti kuhusu uamuzi huo, baada ya Mbunge wa Jimbo la Nzega Vijijini, Dk. Hamis Kigwangala, kupendekeza nchi za Afrika kuwekeza zaidi katika sekta ya afya ili kuwahakikishia wananchi wake wote huduma bora na sio kutegemea wafadhili.

Nipashe ilitembelea akaunti mbalimbali za USAID na kubaini kutokuwapo hewani tangu Februari 4, mwaka huu tovuti na kurasa za mitandao ya kijamii hazikuwa na maudhui yoyote na jana tovuti ilikuwa na taarifa kuhusu mpango wa kuwapumzisha wafanyakazi wake.

Kupitia ukurasa wake wa X, Dk. Kigwangala alisema muda wa kutegemea wafadhili umepita na kwamba ni lazima nchi hizo zibuni mbinu mpya na za kisasa za kugharamia afya za watu wake.

Alisema, kupungua kwa fedha za wafadhili katika sekta ya afya barani Afrika ni changamoto kubwa inayohitaji hatua za dharura kutoka kwa serikali za bara hilo.

Alisema ni muhimu kuwa na mkakati madhubuti kama wa bima ya afya kwa wote, kodi maalum za kulipia bima kwa watu wasio na uwezo pamoja na kuhakikisha kila mtu anakuwa na bima ya afya.

Dk. Kigwangala ambaye ni mtaalamu wa afya ya jamii mwenye Shahada ya udaktari wa binadamu na Shahada ya Uzamili ya afya ya jamii (MPH), alishauri kuwa na utaratibu mzuri wa matumizi ya rasilimali kwa uwazi, ubunifu na uwajibikaji ili kuboresha mfumo wa afya na kupunguza utegemezi wa misaada ya nje.

Kupitia akaunti zake hizo za kijamii, Dk. Kigwangala alipendekeza mbinu za kisasa za kugharimia afya za watu ikiwa ni pamoja kila Mtanzania kuwa na bima ya afya.

"Kwa Tanzania watu wasio na uwezo ni asilimia 26.4 sawa na watu milioni 16.3, kama hao watahitaji kuchangiwa na serikali, fedha Sh. trilioni 2.445 sawa na Sh.150,000 kwa kila mtu.

"Sheria ya bima ya afya kwa wote namba 13 ya mwaka 2023, kwenye kifungu cha tano, tayari inalazimisha kila Mtanzania kuwa na bima ya afya, bila kujumuisha watu wengi, mfumo unaweza kuwa dhaifu kifedha na kushindwa kufanikisha huduma bora kwa wote," alisema Dk. Kigwangala.

Alipendekeza kwamba bima ni lazima itoe huduma muhimu za afya ikiwa ni pamoja na kinga, matibabu na huduma za dharura, ambazo zinapaswa kuwa za ubora wa juu.

Alisema mfumo wa bima ya afya Tanzania, unapaswa kulinda watu dhidi ya mzigo wa gharama kubwa za matibabu na kwamba chanzo cha fedha kinapaswa kuwa endelevu katika tozo za bima, michango ya serikali na vyanzo vingine vya fedha.

Alipendekeza kwamba, mfumo wa utozaji wa tozo unapaswa kuwa wa haki, wenye kipato kikubwa wachangia zaidi ili kusaidia makundi yenye kipato cha chini.

Kadhalika, alipendekeza kanuni za bima ya afya kwa wote za mwaka 2024 zirekebishwe ili kuweka wazi vyanzo vya fedha kwa ajili ya watu wasio na uwezo, namna ya kuwatambua wasio na uwezo na namna ya kuusimamia mfuko wa watu wa kundi hilo.

Dk. Kigwangala ametoa mapendekezo hayo kutokana na agizo la Rais wa Marekani Donald Trump la kusitisha misaada ya usambazaji wa dawa za Virusi vya Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria (PEPFAR) na miradi mingine.

USAID imetangaza kusitisha baadhi ya mikataba ya Huduma za Kibinafsi (PSCs) na Mikataba ya Huduma ya Ushirika (ISCs) ambayo haijatajwa kuwa ya msingi.

Jana wabunge Democratic nchini Marekani wameandamana wakisema uamuzi huo ni kinyume na uamuzi wa kumteua Mfanyabiashara Elon Musk kuwa Mkuu wa Kitengo cha Ufanisi wa Serikali si sawa kwa kuwa hana mamlaka ya kufungwa kwa shirika hilo.

Mbunge Gerry Connolly akizungumza kwenye maandamano hayo, alisema hakuna mtu yeyote anayeweza kuvunja shirika hilo, bali ni Bunge pekee.

Hata hivyo, Trump amemtetea Musk kuwa hawezi kufanya chochote bila idhini ya Ikulu na hatua ya kuvunjwa kwa shirika hilo amepewa baraka na serikali.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# CCM yashtuka, Rais Samia aelekeza njia kuwavuta vijana

**Augusta Njoji na Paul Mabeja,**

**DODOMA**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimetambulisha wagombea wake wa nafasi ya urais huku kikiweka wazi mikakati mitano ya kuendelea kubaki madarakani huku kipaumbele kikiwa kuondoa tatizo la ajira kwa vijana kwa kuanzisha programu maalum.

Akitaja mikakati hiyo jana jijini hapa kwenye sherehe za miaka 48 ya CCM, Mwenyekiti wa Taifa wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan, alisema kwa miaka mitano ijayo watabaini changamoto mpya na kunyumbulika kwa wakati kuzitatua.

"CCM imebaini changamoto ya tatizo la ajira kwa vijana na inatambua hii ni changamoto ya dunia nzima, tumeanza na mabadiliko kwenye sera ya elimu kama nguzo ya kuwajenga kiujuzi na kiutaalamu watoto wetu," alisema.

Alisema ujuzi huo utawawezesha kunufaika na fursa ajira kwenye maeneo yao.

Pia alisema serikali inaweka programu na mipango mbalimbali ya kuboresha mazingira ya biashara nchini ili kuvutia na kuwa na mitaji ya uwekezaji ndani na nje ya nchi ili waajiriwe na kujiajiri.

"Tunafanya jitihada za makusudi kufanya uwekezaji kwenye michezo, sanaa na burudani na uzoefu kutoka nchi zingine umeonekana sekta hizi zinatoa mchango kiuchumi na zinatengeneza ajira nyingi rasmi na zisizo rasmi," alisema.

Pia alisema zinafanyika jitihada za kukuza ufanisi katika sekta ya utalii na kuimarisha uchumi wa buluu kwa kuwa zimeonesha uwezo mkubwa wa kutoa ajira kwa vijana.

"Serikali imeanzisha programu mbalimbali zenye lengo la kujiajiri mwenyewe na kuajiri wengine, kama programu ya jenga kesho iliyo bora (BBT) kwenye sekta za kilimo, mifugo, madini na nyuki, vijana wanajengewa uwezo wanapewa mitaji na nyenzo," alisema huku akibainisha kuwa programu hizo ndio zinaonesha kesho ya CCM.

"Jambo jingine la kutuhakikishia kesho yetu ni kujenga jumuiya ya vijana ya CCM na kuwajenga vijana kiitikadi ili wajue vizuri siasa ya nchi yetu na misingi ya kuanzishwa CCM. Kesho salama ya chama chetu na nchi yetu itahakikishwa kwa vijana wetu kujengewa uwezo ndani na nje ya nchi ili kujipanga kitaasisi ili kupambana kwa hoja na yeyote mwenye hoja hasi," aliongeza.

Alisema lazima Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) kuimarishwa kimkakati kwa kuwa ni hazina ya CCM kwa kuwajengea uwezo na kupikwa kiitikadi katika mazingira ya sasa.

Kadhalika, alisema kwa kuwa CCM inatekeleza ahadi zake anaamini wananchi wataendelea kuwapa dhamana ya kuongoza serikali zote mbili.

"Tukiangalia kazi tuliyoifanya kipindi hiki, tunaamini kuwa uchaguzi wa mwaka huu hali haitakuwa tofauti, watanzania wataendelea kutupa dhamana ya kuongoza serikali zote mbili," alisema.

Alisema pamoja na hali hiyo, wasibweteke kwa kujiamini kuwa ni chama kikubwa na chenye matumaini makubwa kwenye uchaguzi ujao.

"Tunatimiza miaka 48 kwenye mwaka wenye vuguvugu la uchaguzi mkuu nchini. Tusiruhusu kunyemelewa na kiburi cha kuwabeza wapinzani wetu lakini tusiingiwe na pepo la kuwaogopa. Tuendelee kulinda heshima na imani tuliyopewa na wananchi kuliongoza taifa letu," alisema.

Samia alisema CCM imejipanga kuendelea kutoa uongozi thabiti kwa ustawi wa taifa na haitabadilii itikadi yake ya kuwatumikia watu wote na imani yake ya binadamu wote ni ndugu na Afrika ni moja.

"Kuaminika kwa CCM hakujatokea tu inatokana namna inavyoshughulikia matatizo ya wananchi na utekelezaji wa ahadi yake zilizomo kwenye ilani ya uchaguzi za kujenga uchumi imara, kutatua changamoto za kijamii na kujenga miundombinu mbalimbali ya biashara na uwekezaji, hii ni kete ya imani ya wananchama," alisema.

Aidha, alisema huko waendako wananchi wataipima CCM kwa sera na mipango, kazi wanazofanya. Aliwataka wana CCM kuwafikia na kuwasikiliza wananchi na kutatua changamoto zao na CCM imejipanga na matumizi ya TEHAMA ili kurahisisha mawasiliano. Pia alihimiza viongozi katika kuelekea uchaguzi mkuu waongeze kasi ya kuwatembelea wananchi na wanachama kwa kuwafahamisha namna serikali ilivyotekeleza ilani.

"Mwalimu (Julius) Nyerere aliwahi kusema Rais wa chama chetu anaweza kutoka chama chochote lakini Rais bora atatoka CCM. Nataka niwahakikishie wakati utakapofika kwa kushirikiana na wagombea hawa wenzangu walioteuliwa na timu nzima ya CCM tutapeperusha vyema bendera ya CCM na naimani wananchi watatupa dhamana ya kuendelea kuongoza, CCM Baba lao na Mama lao wengine bado wanafunzi wajifunze," alisema.

Kuhusu uteuzi wagombea ubunge na madiwani, Rais Samia aliwahakikishia wanachama kwamba CCM itatenda haki katika kupata wagombea wanaotokana na CCM na wanaokubalika.

Naye Katibu Mkuu wa CCM na Mgombea Mwenza Mteule, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, alisema atatumia uwezo wake kusaidia kazi alizozianzisha Rais Samia na kuhakikisha hazirudi nyuma.

Pia alisema mafanikio ya utekelezaji ya Ilani ya CCM ya 2020, inampa jeuri ya kuwa tayari kuendelea kufanya kazi chini ya Rais Samia.

"Nina imani kuwa nitafanya kila lililo ndani ya uwezo wangu kuhakikisha kwamba kazi unayoifanya hairudi nyuma, kuhakikisha kwamba nakusaidia kwa nguvu na uwezo wangu wote," alisema.

Alisema pia atashiriki kusaidia kuhakikisha kwamba kasi ya maendeleo ambayo Rais Samia ameyaanzisha yanazidishwa maradufu.

Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, alisema wanachama wanawajibu wa kudumisha mafanikio ya CCM kwa kuimarisha umoja na mshikamano.

"Wana CCM tuna wajibu wa kudumisha misingi ya chama chetu na kuzidi kuimarisha chama chetu kwa kuendelea kushika dola za serikali zote mbili na tunawajibu wa kuhamasisha wanachama wetu kujiandikisha kwenye daftari la wapigakura na wakati ukifika wanakwenda kuichagua CCM," alisema.


14th January, 2025

**REF. NO. FHF/CRD/1344/2025**
**Land Form No. 54 A**

**RE: NOTICE OF DEFAULT**
***(Made Under Section 127 of the Land Act Cap 113 [R: E 2019)***

**C.T NO. 67284 LR Mwanza,**
**PLOT NO. 540, BLOCK 'M',**
**BUHONGWA,**
**MWANZA CITY.**

**To:**
**Meggyresta Kiariro Mweta,**
**P.O. Box: 7445,**
**Mwanza,**
**Tanzania.**

Dear Sir,

This is to notify you of your default to honour your obligations, covenanted under the Mortgage Deed and the loan agreement/ Term Loan/ Credit Facility Agreements dated **7th November, 2023** with Reference Number **FHF/CRD/481/2023.** The Breach of the terms and condition (Covenants) that has prompted First Housing Finance Tanzania Limited to issue the statutory default notice is as follows;

That you defaulted in repayment of instalments and servicing the approved credit facilities on principal plus accrued interest since **14th November, 2024** to date thereof which stands at **TZS 131,371,067.84** as of **14th January, 2025.**

Please note that the amount of accrued interest varies with as days' elapse.

Be further notified that in the event you as a borrower and mortgagor do not rectify the default stated above within Sixty Days (60) from receipt of this notice, the Bank will exercise its rights to sell the mortgaged property cited above, or appoint a receiver, or lease the property, or enter possession.

Dated at Dar es Salaam this 14th January, 2025.

Authorized Signatory

Authorized Signatory

Served upon me on this ………. day of…………………………., 2025.

218365502

HABARI KITAIFA

# Kamati Bunge yashtushwa ongezeko matumizi dawa za kulevya za kemikali

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KAMATI ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria imebaini ongezeko la matumizi ya dawa za kulevya zenye kemikali bashirifu nchini hasa aina mpya ya NPS ambazo zina viwango vikubwa vya kilevi mara 50 hadi 100 ikilinganishwa na dawa zingine.

Kutokana na hali hiyo, Bunge limeazimia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini ishirikiane na Taasisi ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Shirika la Viwango (TBS) na Bohari ya Dawa Tanzania (MSD), kudhibiti maduka ya dawa za binadamu kujihusisha na uuzwaji wa kemikali bashirifu nchini.

Akiwasilisha jana bungeni taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati hiyo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. Joseph Mhagama, alisema kamati imebaini kwa mwaka 2023 Mamlaka ya kuzuia na kupambana na dawa za kulevya nchini ilifanikiwa kuzuia uingizaji nchini wa kemikali bashirifu kilogramu 157,738.55 na kukamata kemikali bashirifu zenye ujazo wa lita 22,682 kwa kipindi cha Januari hadi Septemba 2024.

"Changamoto ya ongezeko la matumizi ya kemikali hizi bashirifu 'NPS' zina viwango vikubwa vya kulevya mara 50 hadi 100 ukilinganisha na dawa za kulevya zinazodhibitiwa kimataifa na hupelekea matatizo makubwa ya afya na athari za magonjwa mbalimbali ikiwamo utegemezi na uraibu usioponyeka kirahisi, magonjwa ya akili, moyo, mfadhaiko, kifafa na vifo vya ghafla kwa mtumiaji," alisema.

Alisema Bunge linaazimia serikali ihakikishe elimu inatolewa kuhusu uwapo wa aina hiyo ya NPS na madhara ya kemikali hizo kwa jamii.

"Kamati inaishauri Mamlaka iendelee kudhibiti na kupambana na uingizwaji wa fawa za kulevya nchini na iendelee kuzishirikisha mamlaka nyingine za serikali kama TBS, TMDA na MSD ili kuhakikisha kwamba, taasisi hizi zinashirikiana kwa pamoja kudhibiti uchepushaji wa kemikali na dawa halali kutumika kinyume na matumizi yaliyokusudiwa (dawa za kulevya)," alisema.

Pia, alisema Bunge linaazimia serikali iongeze bajeti ya mamlaka ili kujenga vituo vya matibabu na msaada wa kisaikolojia kwa waraibu wa dawa za kulevya hadi ngazi ya mkoa.

"Na kuimarisha udhibiti wa uingizwaji wa dawa za

kulevya nchini kwa kutumia mifumo ya kisasa

katika sehemu za usafirishaji na upakuaji mizigo nchini," alisema.

Alisema Bunge linaazimia serikali kupitia kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (MSLAC) na ikishirikiana na Asasi za Kiraia nchini iwafikie wananchi wote nchini hasa waishio maeneo ya vijijini.

Kadhalika, alisema serikali iiwezeshe Tume ya Kurekebisha Sheria kwa kuitengea fungu la maendeleo ili kutekeleza jukumu la kufanya utafiti kwa sheria kabla hazijaletwa bungeni.

"Serikali ihakikishe kwamba inatenga Bajeti ya kutosha kwa Tume ya Kurekebisha Sheria ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu," alisema.

Katika hatua nyingine, alisema serikali iratibu utengenezwaji wa mfumo wa pamoja wa ulipaji kodi (mifumo ya kodi kusomana) kwa wawekezaji na wafanyabiashara nchini.

"Kuwapo kwa mfumo mmoja wa utoaji leseni za biashara nchini kwa wawekezaji wazawa na wa kigeni ambao utaratibiwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania," alisema.

## TBT yakutana na wadau utatuzi changamoto

**Na Halfani Chusi**

BODI ya Chai Tanzania (TBT), imekutana na wadau wa zao hilo nchini kwa lengo la kujadili namna ya kukabiliana na changamoto zinazo wakwamisha.

Baadhi ya changamoto zilizotajwa kukwamisha ni pamoja na kukatika kwa umeme, ubovu wa miundombinu ikiwamo barabara.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Kaimu Mkurugenzi Bodi hiyo, Beatrice Banzi alipokutana na wadau kutoka serikalini, TBT, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), bandari, maofisa kutoka vyama vya ushirika na Wizara ya Kilimo kwa lengo kuangalia namna ya kutatua changamoto hizo.

"Pia tutajadili namna ya kuongeza ubora wa chai ili kulishika soko la chai ndani na nje ya nchi, lakini pia tutafanya hamasa kwa Watanzania wanywe chai kwa wingi na hasa inayozalishwa nchini kwa sababu inaonekana unywaji chai upo chini," alisema Beatrice.

Aidha, alisisitiza lengo lao lingine ni kupanga kwa pamoja ili kufikia malengo waliojiwekea kuendeleza zao hilo kwa muda wa miaka 10 kuanzia mwaka 2024 mpaka 2034.

"Lakini ili kufikia malengo hayo, lazima watu wa serikali, sekta binafsi wakae chini kwa pamoja kujadili ni jinsi gani wanaweza kuokoa zao hilo," alisema na kuongeza:

"Hapa ni kama tunafanya 'road map' ili tuweze kujua tunaendaje, kama ni kuongeza uzalishaji wale wadau wanaohusika na uzalishaji tunapanga kwa pamoja tunafanyaje".

Vilevile alisema: "Kama tunataka kutangaza chai yetu ndani na nje ya nchi tunafanyaje kwa kushirikiana na TANTRADE kwa hiyo yale majadiliano yetu sisi washiriki wa mkutano wa leo ndiyo yatatumika kama 'road map' yakuweza kuboresha huu mkakati ambao tumeupanga kuinua na kuendeleza zao la chai kwa hiyo miaka kumi".

Aidha, alisema katika kikao hicho watatambulisha nembo ya chai ya Tanzania ili iwe rahisi kutambuliwa hata ikiuzwa nje ya nchi na kwamba wanaamini hatua hiyo itasaidia kukuza biashara ya zao hilo.

*Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

## INEC yakumbusha umuhimu kuzingatiwa sheria za uchaguzi

**Na Romana Mallya**

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi imesema ni muhimu kwa watendaji wanaohusika na uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura kuzingatia Katiba, sheria za uchaguzi na kanuni zake katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mjumbe wa Tume hiyo, Jaji Asina Omari, aliyasema hayo juzi wakati akifunga mafunzo ya siku mbili kwa maofisa waandikishaji, maofisa waandikishaji wasaidizi ngazi ya jimbo, maofisa uchaguzi na maofisa TEHAMA mkoani Pwani.

Jaji Asina aliwataka watendaji kuhakikisha kuwa wanaendelea kutumia muda wao wa ziada kusoma na kupitia maelekezo yote waliyopewa ili kuongeza uelewa zaidi kuhusu wajibu na majukumu yao katika mchakato wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

"Ni matarajio ya Tume mara baada ya mchakato huu kukamilika watu watakaokuwa wamepatiwa kadi watakuwa ni wapiga kura halali wa kumchagua Rais, Wabunge na Madiwani," alisema.

Akifunga mafunzo kama hayo mkoani Tanga yaliyohusisha washiriki kutoka katika Halmashauri ya Jiji la Tanga, Halmashauri za Miji ya Handeni na Korogwe, Halmashauri za Wilaya ya Kilindi, Lushoto na Muheza, Mjumbe wa Tume, Magdalena Rwebangira, aliwataka kuhamasisha wananchi wenye sifa kujiandikisha.

Rwebangira alisema jukumu la uhamasishaji linawahusu watendaji moja kwa moja wao, kwa kushirikiana na wadau wengine katika maeneo yao kupitia nyenzo walizonazo.

"Mabango na vipeperushi mtakavyopewa na Tume mvisambaze mapema katika shehia zote zilizoko katika mikoa yote mitatu ya Unguja. Kazi yenu kubwa ni kusimamia na kuendesha shughuli zote za uboreshaji katika shehia zote," alisema.


Jubilee
HEALTH INSURANCE

Hatua Rahisi za Kuishi Kwa Afya Mnamo 2025

**Na Shaban Salehe, Afisa Mkuu wa Uendeshaji**

Kuanza mwaka mpya kunaleta matumaini na fursa ya mwanzo mpya. Hata hivyo, maazimio mengi hupotea ifikapo Februari. Kosa la kawaida ni kuweka malengo makubwa kupita kiasi, kama vile kupunguza kilo 20 kufikia Machi. Badala yake, anza na hatua ndogo zinazoweza kutekelezeka ambazo zitajenga tabia ya kudumu.

Fanya malengo yako kuwa maalum. Tamaduni zisizo na maelezo kama "nitakula kwa afya" hazina mwelekeo. Tumia vigezo Maalum, vinavyoweza kupimwa, vinavyoweza kufikiwa, vinavyohusiana na unachokihitaji, na vinavyopangwa kwa wakati ili kuunda malengo yenye uwazi na yanayoweza kudhibitiwa.

Kumbuka kuwa maendeleo hayapatikani kirahisi. Changamoto za maisha zinaweza kuharibu mipango, lakini vizuizi havipaswi kuzuia safari yako. Pitia na badilisha malengo yako inapohitajika.

Ili kuweka ratiba yako kuwa ya kufurahisha, chagua shughuli zinazokuvutia, kama vile madarasa ya dansi au mazoezi ya viungo. Teknolojia inaweza kusaidia pia; programu kama Maisha Fiti kutoka Jubilee Health Insurance inatoa msaada wa jamii katika changamoto za afya ili kufanya safari yako ya afya iwe ya kuvutia.

Sherehekea kila hatua, hata ikiwa ndogo. Tambua maendeleo yako—iwe ni wiki moja ya mazoezi ya nguvu au hata kutembea tu, kunatia nguvu na hamasa katika kuendelea na kujitolea kwako.

Februari hii, weka malengo ya afya ambayo ni halisi na yenye kuitendea haki nafsi yako. Hata juhudi ndogo zinaweza kuleta mabadiliko makubwa ifikapo Desemba. Hii ni kwa ajili yako, afya bora na furaha zaidi mnamo 2025!

Kujua zaidi kuhusu programu zetu za afya na Maisha Fiti App, wasiliana nasi kupitia **www.jubileetanzania.co.tz** au **0748500877.**



Shaban Salehe, Afisa Mkuu wa Uendeshaji

183647

TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

# MWITO WA KUTOA MAONI KUHUSU MAOMBI YA VIBALI VYA UJENZI NA LESENI KUTOKA EWURA

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 126 (1) cha sheria hiyo kinamtaka mtu yoyote anayetaka kujenga miundombinu ya mafuta kuomba kibali cha ujenzi kutoka EWURA. Aidha, Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

EWURA imepokea maombi ya vibali vya ujenzi na leseni kutoka kwa waombaji walioorodheshwa hapa chini. Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba vibali vya ujenzi ili wajenge miundombinu ya mafuta na leseni kwa ajili ya kujihusisha na biashara/shughuli katika mkondo wa kati na chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Ombi la Leseni/Kibali cha Ujenzi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Leo Plastics Limited, S. L. P 896, Arusha. | Kiwanja Na. 14, Kitalu "BB", Eneo la Viwanda la Themi, Arusha. | Sandesh Kumar Aggawal (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 2. | Asas Transporters Company Limited, S. L. P 562, Iringa. | Kiwanja Na. 31/2 Barabara ya Mandela, Eneo la Tabata, Ilala, Dar es Salaam. | Ahmed Faraj Abri (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 3. | Afrisian Ginning Ltd, S. L. P 19964, Dar es Salaam. | Eneo la Misugusugu, Kibaha, Pwani. | Samir Abdulwahid (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 4. | Backtown Transport Company Limited, S. L. P 16476, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 6, Kitalu "J", Pingo, Chalinze, Pwani. | Hussein Riadha Talecky (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 5. | Kamal Refinery Limited, S. L. P 10392, Pwani. | Kiwanja Na. 84, Kitalu "M", Eneo la Kerege, Bagamoyo, Pwani. | Sameer Santosh Gupta (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kiwanda cha Kutengeneza Vilainishi (*Lubricant Blending Plant*) |
| 6. | Buti la zungu petrol station, S. L. P 578, Lindi. | Kiwanja Na. 1, kitalu "F", Eneo la Kiduni, Lindi. | Zuberi Bakari Juma (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 7. | Robert Burchard Kaiqwa, S. L. P 103, Karagwe. | Kiwanja Na. 187, Kitalu "D", Eneo la Omurushaka, Karagwe, Kagera. | Robert Burchard Kaiqwa (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 8. | Kasenene Company Limited, S. L. P 103, Karagwe. | Kiwanja Na. 21, Kitalu "K", Eneo la Kayanga, Karagwe, Kagera. | Mwesige Kasenene Rwiza (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 9. | Wilfred Masanja Mahizi, S. L. P 14202, Dar es Salaam. | Eneo la Wishiteleja, Kishapu, Shinyanga. | Wilfred Mahizi Masanja (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 10. | Barthomeo Christian Manunga, S. L. P 94, Chato. | Kijiji cha Nyarutembo, Chato, Geita. | Barthomeo Christian Manunga (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 11. | Zuberi Saidi Maeda, S. L. P 167, Nkasi. | Kijiji cha Isasa, Nkasi, Rukwa. | Zuberi Saidi Maeda (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 12. | Acer Petroleum (T) Ltd - Nzovwe S. L. P 78845, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.1035, Kitalu "R", Nzovwe, Mbeya. | Atul Mittal (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 13. | Neema Mulinga Nyalege, S. L. P 1126, Chamwino. | Kijij cha Zajilwa, Chamwino, Dodoma. | Neema Mulinga Nyalege (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 14. | ET & T'S Investments Ltd - Samanga Marangu Petrol Station, S. L. P 780, Marangu. | Eneo la Samanga Marangu, Moshi Kilimanjaro. | Eliawony Godfrey Towo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 15. | Arthur Fidelis Mushi-Gallapo service station, S. L. P 12049, Arusha. | Kiwanja Na. 86, Kitalu "A", Eneo la Gallapo, Babati, Manyara. | Arthur Fidelis Mushi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 16. | RM Petrol Station - Kibirashi, S. L. P 18, Kilindi. | Kijiji cha Kibirashi, Kilindi, Tanga. | Ramadhani Maulidi Mrisho (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 17. | Mshangama Ayoub Mzee T/A Mnazi Filling Station, S. L. P 1973, Tanga. | Kijiji cha Kwemkwazu, Lushoto, Tanga. | Mshangama Ayoub Mzee (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 18. | Afroil Investment Limited, S. L. P 38383, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "E" Eneo la Mnadani, Mbwanga, Dodoma. | Hilmy Ahmed Mbarak (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 19. | Afroil Investment Limited, S. L. P 38383, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 113 &, 97, Eneo la Mnadani, Dodoma. | Hilmy Ahmed Mbarak (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 20. | Afroil Investment Limited, S. L. P 38383, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 26, Kitalu "AA" Eneo la Kikuyu Mashariki, Dodoma. | Hilmy Ahmed Mbarak (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 21. | Puma Energy Tanzania Limited, S. L. P 9043, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 168, Eneo la Msalato, Dodoma. | 1. Puma Investment Limited (UK) 2. Serikali ya Tanzania | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 22. | Landmark Filling Station - Kibaigwa, S. L. P 64, Kongwa. | Kiwanja Na. 1, Eneo la Mandela - Kibaigwa, Kongwa, Dodoma. | Fatuma Ramadhani Mganga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 23. | Donald Simango Mejiti, S. L. P 2993, Dodoma. | Kijiji cha Mpwayungu, Chamwino, Dodoma. | Donald Simango Mejiti (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 24. | Seleman Tullo Mdoe T/A Kwesine Petroleum, S. L. P 45370, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "J", Eneo la Ilongeroi, Singida. | Seleman Tullo Mdoe (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 25. | Hero Retail Limited, S. L. P 391, Singida. | Kiwanja Na. 322 & 323, Kitalu "HH", Eneo la Mwenge, Singida. | Abdi Hakim Ibrahim (Raia wa kenya) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 26. | Yusuph Amani Maimu - Dutumi Oil Service Station, S. L. P 90005, Dar es Salaam. | Eneo la Dutumi, Morogoro. | Yusuph Amani Maimu (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 27. | Unique Petroleum Tanzania Ltd, S. L. P 119, Tabora. | Kiwanja Na. 455, Kitalu "D", Eneo la Isevya, Tabora CBD, Tabora. | Shaffin Sumar (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 28. | Hero Retail Limited, S. L. P 1630, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 14, Kitalu "A", Eneo la Ujenzi, Kigoma CBD, Kigoma. | Abdi Hakim Ibrahim (Raia wa kenya) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 29. | Ngabanya Gillu Migangala T/A Nyabanya Filling Station, S. L. P 36, Kahama. | Kiwanja Na. 81 & 83, Kitalu "A", Eneo la Masumbwe, Mbogwe, Geita. | Ngabanya Gillu Migangala (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 30. | TANOIL Geita Station, S. L. P 1191, Dodoma. | Kiwanja Na. 171, Kitalu "E", Eneo la Kalangalala, Geita. | James Sanawa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

Inaendelea Uk. 5

183658

# TANGAZO

Inatoka Uk. 4

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Ombi la Leseni/Kibali cha Ujenzi |
|---|---|---|---|---|
| 31. | Tilu A. Nsimba T/A ABG Service Station, S. L. P 22, Katoro. | Kiwanja Na. 482, Kitalu "A", Eneo la Katoro, Geita. | Tilu A. Nsimba (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 32. | Hero Retail Limited, S. L. P 1630, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 364, Kitalu "G", Eneo la Bomani, Tarime, Mara. | Abdi Hakim Ibrahim (Raia wa kenya) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 33. | Virian Oil Limited, S. L. P 246, Bunda. | Kiwanja Na. 27 & 29, Kitalu "N", Bunda, Mara. | Marwa Chogo Marwa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 34. | Valeriani John Ottaru, S. L. P 403, Bunda. | Eneo la Oshashi, Bunda, Mara | Valeriani John Ottaru (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 35. | Kanyigo Filling Station, S. L. P 160, Kanyigo. | Kiwanja Na. 49KANGOI, Kitalu "168KT", Eneo la Kanyigo, Missenyi, Kagera. | Salim Mbaziila (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 36. | Gyunda General Supply, S. L. P 89, Ngara. | Kijiji cha Mukikomero, Ngara, Kagera. | Deogratius Nicholauce Kidenke (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 37. | KM Energy, S. L. P 59, Ngara. | Kijiji cha Mugoma, Ngara, Kagera. | Kalist Stanslaus Mboya (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 38. | Projectus Bendabenda Rutinwa, S. L. P 131, Muleba. | Eneo la Kyebitembe, Muleba, Kagera. | Projectus Bendabenda Rutinwa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 39. | Nyamse Petrol Station - Ngulyati, S. L. P 200, Magu. | Kijiji cha Ngulyati, Bariadi, Simiyu. | Hassan Hamis Nyamse (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 40. | Simiyu Investment Company Limited, S. L. P 105, Meatu. | Kiwanja Na. 110, Kitalu "C", Eneo la Mwandoya, Meatu, Simiyu. | Ntemi Daud Mpina (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 41. | GBP Tanzania Limited, S. L. P 6185, Mwanza. | Kiwanja Na. 260, Kitalu "W", Eneo la Bukala, sengerema, Mwanza. | Badar Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 42. | Deus Clement Kiyela, S. L. P 351, Geita. | Eneo la Ibisabageni, Sengerema, Mwanza | Deus Clement Kiyela (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 43. | Hass Petroleum (T) Limited - Iyunga, S. L. P 78341, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 239, Kitalu "LL", Eneo la Iyunga, Mbeya. | Abdirahman Mohamed (Raia wa Kenya) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 44. | Kilimanjaro Truck Company Limited S. L. P 80478, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 228, Mpemba, Tunduma, Momba, Mbeya. | Rowland Patrick Sawaya (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 45. | Njombe Filling Station Company Ltd - Mbeya Meta S. L. P 411, Njombe. | Kiwanja Na. 1421, Kitalu "M", Eneo la Forest, Mbeya. | James Malika Mwinuka (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 46. | Petroafrica (T) Limited-Iwambi Service Station, S. L. P 4878, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "E", Eneo la Iwambi, Mbeya. | Yassin Warsame (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 47. | Puma Energy (T) Limited-Puma Mbeya Service Station, S. L. P 9043, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1A, Kitalu "B", Barabara ya Karume, Mbeya. | 1. Puma Investment Limited (UK) 2. Serikali ya Tanzania | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 48. | Saatatu Investment Limited, S. L. P 14, Mbozi. | Kiwanja Na. 171 & 182, Kitalu "A", Eneo la Mwaka, Momba, Songwe. | Yona Saatatu Chaula (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 49. | Afroil Investment Limited S. L. P 38383, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 5, Kitalu "K", Mpemba, Tunduma, Momba, Songwe. | Hilmy Ahmed Mbarak (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 50. | Tawaqal and Company (1995) Ltd - Sabasaba Service Station, S. L. P 155, Sumbawanga. | Kiwanja Na. 110, Kitalu "E", Eneo la Sabasaba, Mazwi, Sumbawanga, Rukwa. | Aziz Mohamed Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 51. | Mabena Enterprises Company Limited - Mabena Petrol Station, S. L. P 710, Songea. | Kiwanja Na. 150, Kitalu "B", Eneo la Nundu, Njombe. | Amos Site Mabena (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 52. | Felisiani Selestin Mgaya T/A Mgaya Tiles, S. L. P 761, Songea. | Kiwanja Na. 282, Kitalu "FF", Msamala, Songea, Ruvuma. | Felisiani Selestin Mgaya (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 53. | Oryx Energies Tanzania Limited, S. L. P 9540, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2/2, Eneo la Kurasini, Temeke, Dar es Salaam. | 1. Overseas Petroleum Holdings (UK) 2. Oryx Energies SA (*Switzerland*) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 54. | Hass Petroleum(T)Ltd, S. L. P 78341, Dar es Salaam. | Eneo la Vijibweni, Kigamboni, Dar es Salaam. | Abdulkadir Hussein (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 55. | Zebra Oil Company Limited, S. L. P 76173, Dar es Salaam. | Eneo la Mikocheni, Kinondoni, Dar es Salaam. | Zhonggeng Zhuang (Raia wa China) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 56. | Lubevo Co. Limited, S. L. P 13989, Dar es Salaam. | Eneo la Tabata Matumbi, Ilala, Dar es Salaam. | Ayman Hijaz (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Vilainishi (*Lubricants*) |
| 57. | Alpha Energy Tanzania Limited, S. L. P 9673, Dar es Salaam. | Eneo la Mbagala, Temeke, Dar es Salaam. | Owen Gowell (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Vilainishi (*Lubricants*) |
| 58. | Yamuna Petroleum Limited, S. L. P 19023, Dar es Salaam. | Eneo la TAZARA, Temeke, Dar es Salaam. | Pratik Masrani (Raia wa India) | Leseni ya Jumla ya Vilainishi (*Lubricants*) |
| 59. | SKEU Investment Company Limited, S. L. P 6678, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2048, kitalu "E", Eneo la Ukonga Madafu, Ilala, Dar es Salaam. | Stellah Kabaka Melkiony (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 60. | Utahiza Oil and Gas Company, S. L. P 3864, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P19017, Eneo la Tandika, Temeke, Dar es Salaam. | Yussuf Salim Yussuf (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 61. | GBP Tanzania Ltd-Africana Service Station, S. L. P 3728, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 4, Kitalu "C", Eneo la Mbezi Africana, Kinondoni, Dar es Salaam. | Badar Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 62. | Sayari Filling Station - Mpiji Magohe, S. L. P 354, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P757, Eneo la Mpiji Magohe, Kinondoni, Dar es Salaam. | Leonard Nicolaus Mirenyi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 63. | Mount Meru Petroleum Ltd - Buza, S. L. P 78845, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 422, Kitalu "E", Eneo la Yombo Vituka, Temeke, Dar es Salaam. | Atul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 64. | Joseph Philip Mmewa-Sadani Oil, S. L. P 80600, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 173, Kitalu "H", Eneo la Kivule, Ilala, Dar es Salaam. | Joseph Philip Mmewa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 65. | National Oil Tanzania Ltd-Bagamoyo, S. L. P 70048, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 362, kitalu "R", Eneo la Ukuni, Bagamoyo, Dar es Salaam. | Moteza Augustine Mushi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 66. | Donasian Cornel Mkusu, S. L. P 55068, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 171, Kitalu "4", Kwembe, Mbezi, Ubungo, Dar es Salaam. | Donasian Cornel Mkusu (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 67. | Top Oil Pugu Kajiungeni, S. L. P 42445, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2686, Kitalu "H", Eneo la Pugu Kajiungeni, Ilala, Dar es Salaam. | Mbarak Salim Bawazir (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 68. | Animal Care Company Ltd, S. L. P 55010, Dar es Salaam. | Eneo la Vikuruti-Mlandizi, Kibaha, Pwani. | Hafidh Hamdoun Mansour (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 69. | Saturn Corporation Limited, S. L. P 77007, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2-11, Kitalu "B", Eneo la Kisarawe II, Kigamboni, Pwani. | Chirat Kiritkumar Tanna (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 70. | Silasi Mayunga Masalu T/A Vatican Investment, S. L. P 21022, Pwani. | Kiwanja Na. 1 & 2, Eneo la Kibaha Mwendapole, Kibaha, Pwani. | Silasi Mayunga Masalu (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 71. | Offshore Partners Tanzania, S. L. P 23201, Dar es Salaam. | Eneo la Bandari, Mtwara Mikindani. | Michael Kimei (Mtanzania) | Leseni ya *Condensate Dealership* |

***Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote aliyetajwa hapo juu kwamba asipewe leseni au Kibali cha ujenzi, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.***

***Imetolewa na***
***Mkurugenzi Mkuu,***
***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# CCM imeonesha ukomavu kwa miaka 48 ya uhai wake

**CHAMA** Cha Mapinduzi (CCM) jana kiliadhimisha miaka 48 tangu kuanzishwa mwaka 1977. Chama hicho kilianzishwa baada ya kuunganishwa TANU, chama kilichopigania na kupatikana kwa Uhuru wa Tanganyika (Tanzania Bara) na Afro Shiraz Party (ASP) kilichopigania na kufanikisha Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar mwaka 1964.

Tangu kuanzishwa hadi sasa, CCM imekuwa na utaratibu wa kuchagua viongozi kila baada ya miaka mitano ndani ya chama, hivyo kuonesha kwa dhati kuwa kinadhihirisha demokrasia ya kweli na kuwa chama kiongozi katika kutekeleza jambo hilo na utawala wa sheria.

Kila unapofika wakati wa uchaguzi ndani ya chama, hufanyika mchakato kwa wanachama kuomba nafasi na majina ya waombaji kujadiliwa katika vikao mbalimbali na hatimaye wenye sifa kupitishwa kwa ajili ya kugombea katika uchaguzi mkuu kwenye ngazi husika.

Licha ya kufanya uchaguzi na kuwezesha viongozi kubadilishana na kupozana madaraka kwa njia ya ushindani wa wazi, CCM pia imekuwa mfano bora si kwa Tanzania tu bali kwa Afrika kuwa chama chenye nia ya dhati ya kudumisha demokrasi na utawala bora. Viongozi wa juu, kwa maana ya Rais wa Tanzania na Zanzibar, wakimaliza vipindi viwili vya miaka mitano kila kimoja, huachia madaraka na kupisha wengine kuwania nafasi za urais kwa njia ya ushindani.

Katika muktadha huo, tangu kuanza kwa uchaguzi mkuu unaohusisha vyama vingi mwaka 1995, kumekuwa na idadi kubwa ya wanachama wanaojitokeza kwa wingi kwa ajili ya kuwania nafasi hiyo.

Mwaka 2005 kwa mfano, walijitokeza wanachama 11 kuwania nafasi ili kumrithi aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa. Pia mwaka 2015, walijitokeza wanachama 28 kumrithi Jakaya Kikwete, hali ambayo inaonyesha kukomaa kwa demokrasia ndani ya chama hicho tawala. Hali hiyo ni tofauti na baadhi ya vyama ambavyo vimekuwa ama vikipendekeza mtu mmoja kuwa mgombea au kiongozi mkuu wa chama husika kujitangaza kuwa ndiye mgombea.

Mbali na demokrasia, CCM imekuwa ikikemea rushwa na kufuatilia kwa kina utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika kipindi husika kupitia miradi ya maendeleo ya uondoshaji wa kero za wananchi. Mwaka 2013, kwa mfano, sekretarieti ya CCM iliyokuwa chini ya aliyekuwa Katibu Mkuu, Abduklrahman Kinana, ilizunguka nchi nzima na kukutana na kero mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Kutokana na kuwapo kwa kero hizo, viongozi hao waliwaita baadhi ya mawaziri ambao kero zilihusu wizara zao na kuhojiwa kwa nini mambo hayo yanaendelea na hakuna hatua zinazochukuliwa. Hali hiyo pia ilisababisha mawaziri waliokuwa wakihusishwa na kero hizo, kuitwa 'mawaziri mizigo', hivyo kupendekeza kwa Rais kuwachukulia hatua.

Pamoja na hayo, CCM imeendelea kusisitiza viongozi wanaopewa dhamana kutatua kero za wananchi badala ya kudhani kuwa wako kwenye nafasi hizo kwa manufaa binafsi. Hiyo imekuwa ikisisitizwa kuanzia ngazi ya taifa hadi mtaa na kijiji kila kiongozi awajibike kuhakikisha wananchi wanapata maendeleo.


Kwa ujumla, CCM imedhihirisha kuwa imekomaa katika kudumisha demokrasia, utawala bora, haki na usawa kwa wananchi bila kujali itikadi na imani zao. Kwa sasa, kutokana na kusimamia maendeleo ya wananchi katika sekta mbalimbali, CCM imeonesha kuwa bado kimbilio la wengi katika maendeleo ya nchi. Hali hiyo imejidhihirisha katika uchaguzi mbalimbali kwa kushindwa kwa kishindo.

Wahenga wanasema barabara ndefu haikosi kona. Ni ukweli kwamba chama hicho kimeonesha kuwa kikongwe lakini kuna kasoro kadhaa ambazo zimekuwa zikikwamisha uhuru na demokrasia. Hata hivyo, kasoro hizo haziifanyi kionekana chama dhaifu kulinganisha na vingine vilivyoasisiwa rasmi kuanzia mwaka 1992 baada ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Hili likomeshwe wauza maji, juisi wakitumia chupa chafu

**KATIKA** jamii ya Kitanzania, mtaani tunakotajiwa kuwapo mzigo mkubwa wa majukumu ya kutafuta riziki, kuna kundi kubwa la vijana waliozama katika shughuli inayojulikana kama 'Machinga.

Huo ni uchuuzi mdogo uliojiri kundi kubwa la vijana na hasa mijini, ingawa vijijini nako si haba hivi sasa!

Wanaozama katika eneo hilo la uchuuzi, moja ya bidhaa zao kuu ni uuzaji wa maji ya kunywa.

Kutokana na hali halisi ya maisha, pia kimazingira, baadhi ya mikoa nchini kunashuhudiwa kuwapo joto kali, ikiwamo majiji kama ya Dar es Salaam na Tanga, hata tunapovuka bahari kuhamia Unguja na Pemba, kote kuna joto kali, hasa katika misimu husika.

Katika hilo, kundi kubwa la watu linahitaji maji kwa kiu, hata kuwa mtindo wa maisha ya kisasa, huku aina nyingine ya kumiminika, kuna juisi.

Niseme katika msimu huu wa matunda, wapo wanaouza matunda na wapo wanaotengeneza juisi. Kumekuwapo matunda ya aina mbalimbali kwa wingi katika masoko, hivyo watu hufanya biashara ya kuuza juisi na matunda yake.

Sasa kuna ubunifu wa ziada ambao unanipa maswali magumu kiafya na kiusalama, ndani ya joto hilo kali linalowaletea watu kiu; chupa za maji zilizotumika, zinasuuzwa na kutumika tena, wateja nao wanajitosa kununua maji hayo.

Ndicho walichonacho baadhi ya wauzaji juisi, kama walivyo wenzao wa maji, wamekuwa wakiuza zilizowekwa katika chupa za plastiki zenye maandishi mbalimbali ya bei, kinywaji kikiuzwa kati shilingi 500, hadi 200 hata kufika shilingi 100.

Hao wauzaji pia, juisi na maji yao unakuta chupa hawanunui katika maduka, wengi wanaokota katika vyanzo kama kuvizia penye sherehe, wanazikusanya na kuzitumia kwa ajili ya kuweka juisi na maji hayo.

Pia, wapo wanaookota chupa mitaani na kuwapelekea wauza juisi na maji kwa ajili ya kufanyia biashara. Hapo usalama wa afya ya mtumiaji juisi na maji unasimamia wapi?

Inasikitisha, kwa sababu kuna mbadala salama, hivi sasa yapo maduka mengi yanayouza vifungashio vya kila biashara.

Hivyo, inatakiwa tuboreshe biashara kupitia vifungashio hivyo. Zipo glasi na vikombe ambavyo hutumiwa na wateja, kisha wanavyotupa.

Niseme, wafanyabiashara wanaweza kutumia vifungashio hivyo na sio kutumia chupa ambazo baadhi zinakuwa zimetupwa katika maeneo yasiyofaa, halafu zinaokotwa na kupelekwa kufanyia kazi hiyo.

Pia ufike hatua, mjasiriamali aone kasoro, penye huduma za kukaa, zikitumika glasi zinaweza kutumika, zinaoshwa na kuendelea kutumiwa, tofauti na chupa hata zinapooshwa.

Si ajabu, hata kama zimeoshwa bado mapungufu huwa yanakuwapo kwa chupa zilizookotwa.

Hivyo, hapo inatupatia nadharia kwamba, chupa za kuokota ni mitihani kwa afya ya watumiaji, iwe maji au juisi.

Labda tutasafiri mbali na hilo, katika namna ya kujiondoa nayo na sababu iko wazi kuwa imebeba masilahi ya watu, ndugu zetu machinga.

Ni mahali sahihi kwa mamlaka za kiserikali, hasa zinazohusika na afya kuweka mkakati kwa kushirikiana na dola kuu, kukabili hatari hizo kabla hatujafika pabaya.

Katika mfano mdogo, hata tunavyopiga kelele katika mazingira fulani kuhusu magonjwa ya kuambukiza, maana inazama kwa mazingira hatarishi ya maradhi ya kuambukizana kwa namna hiyo.

HABARI KITAIFA

# Mgogoro wa ardhi kumfikisha DC kortini

**Na Onesmo Kapinga**

SAKATA la mgogoro wa ardhi katika eneo la Shule ya Msingi na Sekondari Zavala, Kata ya Buyuni, jijini Dar es Salaam limechukua sura mpya baada ya baadhi ya wananchi kuamua kwenda mahakamani kufungua kesi kudai wanachoita "haki".

Ni umauzi uliofikiwa baada ya Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, kuwapa mwezi mmoja kubomoa nyumba zao walizojenga katika eneo hilo linalodaiwa kuwa ni shule hizo.

Mkuu wa Wilaya alitoa amri ya kuwataka wananchi wa eneo hilo kubomoa nyumba zao Januari 23, mwaka huu wakati wa kikao kilichofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Wiki iliyopita amri hiyo ya mkuu wa wilaya ilianza kutekelezwa, huku baadhi ya wananchi wakidai inafanyika kinyume cha maagizo yake kwa kuwa mazungumzo kati ya pande mbili hayajafikia mwisho.

Mmoja wa waathirika aliyebomolewa nyumba zake tatu, Richard Amos alisema kutokana na tukio hilo, anakusudia kufungua kesi katika Mahakama Kuu ya Tanzania kudai haki yake.

Amos alidai kuwa katika kikao chao na mkuu wa wilaya, walishindwa kuelewana kutokana na kusimamia upande mmoja na wao kukosa nafasi ya kujitetea kuhusiana na jinsi walivyopata eneo hilo, hivyo yeye na wenzake wamekubaliana kwenda mahakamani.

"Mkuu wa wilaya hayuko juu ya sheria, sisi tumeamua kwenda mahakamani kufungua kesi ili mahakama iweze kutafsiri sheria," alidai Amos.

Akizungumzia mgogoro huo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya Ilala, Katibu Tawala wa Wilaya ya Ilala, Charangwa Makwiro, alisema wananchi walionunua viwanja katika eneo hilo watapeliwa.

Charangwa alisema kuwa baada ya kikao cha wananchi na mkuu wa wilaya, walitakiwa kuonana naye ili awasaidie katika masuala ya kisheria, hata hivyo, wananchi hao hawakwenda baada ya kuwa na msimamo wa kwenda mahakamani.

Shabani Haruna, mmoja wa waathirika wa ubomoaji huo, alidai "uamuzi wa kubomoa nyumba za watu ni ubabe wa madaraka wa mtu mmoja, hivyo tunakusudia kwenda mahakamani kutafuta haki."

Haruna alidai kuanza kubomoa nyumba za watu ilhali kulikuwa na mazungumzo yaliyokuwa yanaendelea kati yao na mkuu wa wilaya, kumewashangaza.

Katibu wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Ilala, Mtiti Jilabu, alimwomba Mkurugenzi wa Jiji hilo, Elihuruma Mabelya, kushughulikia haraka mgogoro wa ardhi ulioibuka katika eneo hilo ambalo inadaiwa mmiliki wake halali ni George Chawala.

Mgogoro huo umeibuka baada ya mmiliki wa sasa wa eneo hilo, Shabani Haruna, maarufu Mapete, anayedaiwa kulinunua kutoka kwa Chawala kisha kukata viwanja na kuwauzia watu mbalimbali ambao wamejenga makazi ya kudumu.

Mapete alidai kuwa alilinunua kutoka kwa Chawala zaidi ya miaka mitatu iliyopita, naye Chawala alilinunua kwa Musa Nyemba mwaka 2000, kulingana na hati ya mauziano aliyoitoa mnunuzi wa pili.

KESI MAUAJI KATIBU CCM

## Mahakama yaahirisha hadi Feb. 17 kusubiri upelelezi

**Na Waandishi Wetu, IRINGA**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Iringa imeahirisha kesi ya mauaji ya aliyekuwa Katibu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kilolo, Christina Kibiki hadi Februari 17 itakapotajwa tena kutokana na upelelezi wa kesi hiyo kutokamilika.

Akiomba kuahirishwa kwa kesi hiyo juzi, Wakili wa Serikali, Atupele Makoga, alisema kuwa wanaomba kesi hiyo ipangwe siku nyingine ili waweze kukamilisha upelelezi wa kesi hiyo.

Wakili wa utetezi, Barnabas Nyalusi kutoka kampuni ya mawakili ya BLS Attorney &Partner, aliiambia Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Wilaya ya Iringa, kuwahimiza upande wa Jamhuri kuharakisha upelelezi wa kesi hiyo kutokana na siku 90 walizopewa kisheria kukabia kuisha.

Wakili Nyalusi alidai mbele ya mahakama kuwa kesi hiyo inasikilizwa na kufuatiliwa na jamii kwa ukaribu na kwamba ni vema mchakato wa upelezi ukakamilika haraka ili ianze kusikilizwa.

Kutokana na maombi hayo ya upande wa Jamhuri, Hakimu Mkazi Mfawidhi Mahakama ya Wilaya ya Iringa, Adelina Ngwaya, aliahirisha kesi hiyo.

Waliofikishwa mahakamani hapo ni pamoja Boniphace Ugwale, ambaye ni Diwani wa Kata ya Nyanzwa Kilolo, Kefa Wales, Silla Kimwaga, Willy Chikweo na Hedikosi Kimwaga kwa pamoja wanashtakiwa kumuua Christina Kibiki.

Washtakiwa hao wanadaiwa kutenda kosa hilo Novemba 12, 2024 katika Kijiji cha Ugwachanya, Wilaya ya Iringa Vijijini.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA PWANI NA TANGA KATIKA HALMASHAURI ZA WILAYA ZA LUSHOTO, KILINDI, MUHEZA, KOROGWE, MJI WA KOROGWE, MJI WA HANDENI NA JIJI LA TANGA.

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Pwani na Tanga katika Halmashauri za Wilaya za Lushoto, Kilindi, Muheza, Korogwe, Miji ya Korogwe na Handeni na Jiji la Tanga tarehe 13 hadi 19 Februari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unafanyika kuanzia siku ya Alhamisi tarehe 13 hadi siku Jumatano tarehe 19 Februari, 2025,
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji,
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi ambao hawakuwahi kuandikishwa hapo awali, na ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
2. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi (Jimbo au Kata).
3. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
4. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
5. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili kwa pamoja, wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la Kata anayokusudia kuhamia, kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo katika kituo cha kuandikisha Wapiga Kura ili kukamilisha taratibu na kupatiwa kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) anaweza kuingia kwenye mfumo wa OVRS kwa kupiga *152*00#, kisha, atachagua namba 8 na kubonyeza, kisha atachagua namba 2, kisha atabonyeza namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga simu namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali na hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa tarehe 04 Februari, 2025 na:

Saida H. Mohammed
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

183619



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**TANGAZO LA UUZAJI WA KIWANJA KILICHOPO MBEZI BEACH NAMBA 2172 BLOCK "H" DAR ES SALAAM**

Wanachama wa **State Trading Cooperation Employee Saving and Credit Cooperative Society Limited (STC.SACCOSS),** wanauza kiwanja kilichopo Mbezi Beach chenye ukubwa wa Mita za mraba **2696** hati namba **48957** kilichopo Plot namba **2172 block "H" Dar es salaam.**

Watakaohitaji kununua watume maombi yao na offer zao kuanzia tarehe ya tangazo hili na mwisho wa kupokea maombi hayo tarehe **22/2/2025,** aidha maombi hayo yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

**MKUU WA WILAYA YA KINONDONI**
**1 MTAA WA MINAKI**
**S.L.P 9583**
**14881 DAR ES SALAAM**

Warda A. Obathany
**KATIBU TAWALA WILAYA KINONDONI**

218364902

## RIPOTI MAALUM -2

## STENDI YA MAGUFULI




Mwonekano wa nje wa Kituo cha Mabasi cha Magufuli

# Wataalamu watoa angalizo serikalini wananchi kutozwa huduma ya choo

**Na Christina Mwakangale**

***KATIKA sehemu ya kwanza ya ripoti hii kulikuwa na ushuhuda wa huduma ya choo katika Kituo cha Mabasi cha Magufuli, wilayani Ubungo, Dar es Salaam, ikiwamo kukosekana mahitaji na huduma muhimu kwa watumiaji wanaotozwa ushuru. Endelea na picha pana ya athari zilizoko na undani wake kitaalamu.***

---

Kushindwa kulipa gharama ya huduma ya choo katika kituo hicho cha mabasi kumechangia baadhi ya watumiaji wake kujisaidia holela, ikiwamo kutumia chupa na kuzitupa, jambo ambalo ni hatari kwa afya na mazingira.

Waathirika wakubwa wa gharama hizo ni wale ambao kituo hicho ndiyo sehemu yao ya kujipatia kipato, wakijumuisha madereva wa matoroli na wafanyabiashara ndogo.

Sheria Ndogo za Vituo vya Mabasi na Maegesho ya Vyombo vya Moto za Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo za Mwaka 2022 zinaelekeza adhabu kwa wanaokiuka sheria hiyo, wakiwamo wanaokwenda kulipa huduma ya choo na ushuru wa kiingilio getini.

Sheria inaelekeza "...matumizi ya vyoo na bafu kwenye vituo vya mabasi yatalipiwa kwa viwango vilivyoainishwa. Ni kosa kwa mtu yeyote kuingia katika vituo vya mabasi pasipo kulipia ushuru husika.

"Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya sheria ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia na kama hakuna adhabu maalum iliyoainishwa katika kifungu kilichokiukwa, atatozwa faini isiyopungua Sh. 200,000 na isiyozidi Sh. milioni moja au kifungo kisichopungua miezi 12 na kisichozidi miezi 24 au vyote kwa pamoja (faini na kifungo)."

Hata hivyo, licha ya utozaji huo wa ushuru uliowekewa msisitizo wa kisheria, mwandishi wa habari hii amebaini huduma ya choo iliyoko katika Kituo cha Mabasi cha Magufuli, haikidhi viwango vya kiafya.

Hali hiyo inakinzana na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 inayoelekeza "kila mtu anayeishi Tanzania, atakuwa na haki ya kuwa na mazingira safi, salama na ya kiafya."

Mtaalamu wa Mazingira, Dk. Felician Kilahama, anasema huduma ya choo ni ya msingi, akiwa na angalizo lingine kwamba iwapo kuna gharama za uendeshaji wa huduma hiyo katika maeneo yenye mikusanyiko ya watu kama inavyoshuhudiwa katika Kituo cha Mabasi cha Magufuli, kuwe na vyanzo vingine vya mapato kuendesha huduma hiyo.

"Kuna mtu hiyo Sh. 200 ni kubwa. Uendeshaji huduma ya choo katika vituo vya mabasi uwe unachangiwa na vyanzo vingine. Sh. 200 unaona ni kidogo, lakini kuna ambaye hana kitu, hiyo kwake ni nyingi.

"Fedha si kila kitu lakini afya! Afya ikiwa duni, hata mwenye fedha utagharamika. Mambo yakiharibika, watu wakijisaidia ovyo, kipindupindu kikiingia, kitawakamata wote, watoto na familia yako.

"Iwapo sheria kali kwa wanaojisaidia katika maeneo ambayo si vyoo baada ya huduma hiyo kuwa bure kwa watu wote. Mtu akikamatwa aadhibiwe. Tujifunze unapokuwa na huduma kubwa ya umma, choo ni muhimu. Hata ukienda Mlimani City, choo ni bure, SGR (reli ya kisasa) choo ni bure, uendeshaji



Baadhi ya mitaro katika Kituo cha Mabasi cha Magufuli ilikutwa na haja ndogo iliyohifadhiwa katika chupa: **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE**

huduma ya vyoo katika maeneo hayo unagharamiwa kwa namna nyingine, si moja kwa moja mtu kulipia huduma ya choo," anashauri.

Umoja wa Mataifa (UN) katika kuadhimisha Siku ya Choo Duniani mwaka jana, ulibainisha katika tamko lake kuwa mtu mmoja kati ya watatu kote duniani, hapati huduma ya choo.

UN ilibainisha wastani uliopo duniani kwa ujumla -- mtu mmoja kati ya wanane hujisaidia hadharani, huku watu bilioni 3.6 hawana huduma hiyo, hivyo kusababisha magonjwa kama kipindupindu, kuhara, homa ya matumbo, maambukizi ya minyoo ya matumbo na polio.

Katika maadhimisho ya Siku ya Choo Duniani Novemba 19, 2023 aliyekuwa Waziri wa Afya, Ummy, aliagiza mikoa na halmashauri kutekeleza ukaguzi kwenye kaya, sehemu za jumuiya, maeneo ya biashara na taasisi zote kuhakikisha zinajenga na kutumia vyoo bora.

Pia alielekeza kusimamia vyema Sheria ya Afya ya Jamii na Sheria Ndogo inayohimiza ujenzi, matumizi ya choo bora kwenye ngazi ya kaya, taasisi na maeneo ya jumuiya.

Vilevile, Ummy alielekeza kuhakikisha mamlaka zinasimamia vyema matumizi ya vyoo kwa wasafiri wawapo safarini kwa kuhakikisha mabasi yanasimama kwenye maeneo rasmi, ikiwamo stendi za mabasi na vituo maalum na kupiga marufuku tabia ya wasafiri kujisaidia ovyo njiani, maarufu "kuchimba dawa".

**UZOEFU TRC**

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano Shirika la Reli Tanzania (TRC), Fredy Mwanjala, anasema kwa wastani kwa siku moja watu maelfu, wakiwamo abiria 7,000 hufika kwenye stendi kuu ya usafiri wa reli ya kisasa (SGR) jijini Dar es Salaam.

"Kuna idadi kubwa ya watu wanaofika kwenye kituo hiki cha Dar es Salaam kwa siku. Huduma za choo zinapatikana bure na vyoo wakati wote huwa vinafanyiwa usafi," anasema.

Ujenzi wa Kituo cha Mabasi cha Magufuli uligharimu Sh. bilioni 50.9. Kilizinduliwa rasmi Februari 22, 2021 na Rais wa wakati huo, Dk. John Magufuli.



## Ukosefu 'mochwari' wawashtua viongozi CCM

**Na Oscar Assenga,** MKINGA

MALALAMIKO ya wananchi wa Wilaya ya Mkinga ya kutumia fedha nyingi kutokana na kugharamia gari la kusafirisha wapendwa wao waliopoteza maisha kutoka Maramba kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo) kuwahifadhi, yamekishtua Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Wananchi hao wanadai kutumia gharama kubwa kusafirisha miili hiyo umbali wa kilomita zaidi ya 60 jijini Tanga.

Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Tanga, Rajab Abdallah, akiwa wilayani humo kukagua miradi ya maendeleo, ameshauri serikali kuchukua hatua za haraka kwa kuielekeza Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, kujenga chumba kipya cha kuhifadhia maiti katika Kituo cha Afya Maramba, ili kuwapunguzia wananchi changamoto ya kusafirisha miili hiyo umbali mrefu.

Rajab, alisema kuelekea Maadhimisho ya miaka 48 ya Kuzaliwa kwa CCM, chama hicho kimeamua kushirikiana na serikali kwa kuchangia mifuko 300 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa chumba hicho. Kituo cha Afya Maramba kilijengwa mwaka 1973.

Alisema chumba kilichopo hakikidhi mahitaji na kidogo, hivyo kuna umuhimu wa kuhakikisha wanajenga chumba kipya, ili kiweze kutosheleza na kuondoa changamoto iliyopo sasa.

Aidha, alisema licha ya ujenzi wa chumba cha kuhifadhia maiti, lakini ufanyike utaratibu wa kupatikana nyumba za watumishi kutokana na kwamba jambo hilo limekuwa ni tatizo kubwa kwa watumishi kukaa mbali na maeneo ya kazi.

Awali, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mkinga, Dk. Salvio Wikesi, alisema kituo hicho ni mojawapo ya vituo vikubwa vya afya na kina hudumu zaidi ya wananchi 46,000 huku pia kikipokea wagonjwa kutoka wilaya ya jirani ya Korogwe.

Katika hatua nyingine, mkazi wa Maramba, wilayani humo, Hussein Salehe, aliishauri serikali iendelee na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, ili kuondoa tatizo la wananchi kutafuta huduma mbali.

# Vijiji vyakumbwa uhaba majisafi na vyoo bora

**Na Godfrey Mushi,** HANANG'

VIJIJI 96 vilivyoko katika Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara, vyenye wananchi 368,000 vinakabiliwa na changamoto ya majisafi na ukosefu wa vyoo bora.

Kutokana na hali hiyo, Shirika la WaterAid la Uingereza kwa kushirikiana na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mkoa wa Manyara, limeanza kutekeleza mradi wa mfano Hanang' utakaotatua changamoto hiyo.

Jana, Mkuu wa miradi wa WaterAid Tanzania, Beda Levira, alisema mradi huo unatarajiwa kukamilika Agosti mwaka huu.

"WaterAid katika kutekeleza mradi wa mfano Hanang' utatatua changamoto ya maji safi, vyoo bora na usafi wa mazingira na utanufaisha wakazi 368,000 wa vijiji 96 wa kata 33 za Wilaya ya Hanang'.

"Nia yetu ni kuhakikisha jamii ya eneo hili, inanufaika na mradi wa maji kwa asilimia 100 na kuondokana na magonjwa ambukizi yanayotokana na uchafu wa mazingira na vyanzo vya maji," alisema.

Nchini Tanzania, kulingana na Utafiti wa Hali ya Demografia na Afya pamoja na Utafiti wa Viashiria vya Malaria (TDHS-MIS) wa mwaka 2022, asilimia 18.1 ya kaya zina miundombinu duni ya usafi wa mazingira, huku asilimia 9.7 ya watu wakijisaidia sehemu za wazi.

Mhandisi wa Maji kutoka RUWASA, Barnabas Taligunga, akizungumzia ufumbuzi wa tatizo hilo alisema mradi huo utaongeza nguvu ya uboreshaji wa usafi wa miundombinu ya kusambaza maji kutoka kwenye vyanzo hadi kwa watumiaji.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa huo, Dk. Andrew Method, alitoa wito kwa viongozi wa

> **"Nia yetu ni kuhakikisha jamii ya eneo hili, inanufaika na mradi wa maji kwa asilimia 100 na kuondokana na magonjwa ambukizi yanayotokana na uchafu wa mazingira na vyanzo vya maji," alisema.**

Hanang' kutoa ushirikiano kwa WaterAid kutekeleza mradi huo ili uwe mfano kwa wilaya zingine.

Mkurugenzi Mtendaji na Mipango wa Kimataifa wa WaterAid, Amaka Godfrey, alisema amevutiwa na namna viongozi na jamii ya eneo hilo walivyoupokea mradi huo na namna walivyojiandaa kushiriki katika kuufanikisha.

Amaka alisema mbinu waliyoichagua viongozi ya kufikia jamii katika wilaya hiyo ni nzuri kwani itaweza kufikia watu wengi kwa wakati.

Akichambua matokeo chanya ya ujio wa mradi huo, Mkuu wa Kitivo cha Ushirika na Maendeleo ya Jamii ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Dk. Cyril Komba, alisema vyoo na huduma ya majisafi na salama havipewi umuhimu na jamii, licha ya kuwa ndiyo moja ya vitu vinavyochangia ukuaji wa uchumi.



Katibu wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (MAREMA), Tawi la Mirerani, Rachel Njau (wa pili kulia), akizungumzia na waandishi wa habari Mirerani juzi, wakati akitoa wito kwa wamiliki wa madini ya Tanzanite kufanya minada kila wakati ili kunyanyua kiuchumi eneo hilo. Wengine ni wajumbe wa kamati tendaji ya chama hicho. **PICHA: GIFT THADEY**

## Serikali: Elimu ya uraia, utawala bora iwafikie wananchi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WIZARA ya Katiba na Sheria, imewataka watendaji kuanzia ngazi ya vijiji, kata hadi mkoa, kuwaelimisha jamii kuhusiana na elimu ya uraia na utawala bora inayotolewa na wataalamu ili kuwasaidia wananchi kutambua haki zao.

Mkurugenzi wa Idara ya Katiba na Ufuatiliaji Haki, Jane Lyimo, alielekeza hayo jana, wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo kwa kada hiyo.

Lyimo, alisema wizara hiyo imeona umuhimu wa kutoa mafunzo hayo kwa watumishi hao kuanzia ngazi ya chini hadi juu kwa sababu wanakutana na wananchi hao kila siku katika utekelezaji wa majukumu yao, hivyo ni rahisi kwao kuwafikishia elimu hiyo katika maeneo mbalimbali wanayotoka.

"Tumeamua kutoa mafunzo haya kwa watumishi wa ngazi zote mkoani hapa kwa sababu ni rahisi kwao kuwafikia wananchi kutokana na wao kukutana nao mara kwa mara katika utekelezaji wa majukumu yao," alisema Lyimo. Aidha, alisema wizara hiyo ipo mkoani humo kwa ajili ya kuwaongoza watendaji hao katika ngazi mbalimbali, lengo likiwa ni kutaka wafuate misingi ya utawala bora kwenye utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.


"Tunaamini siku moja tukija Kilimanjaro tutakuta hali imebadilika tofauti na ilivyokuwa miaka mingine kwenye masuala ya utafutaji haki kwa wananchi, ikiwamo kuibadilisha jamii kwenye masuala ya ukatili wa kijinsia,"alisema Lyimo.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Kiseo Nzoa, alisema mafunzo hayo yana umuhimu kwao kama watumishi wa umma kwa sababu ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku kwa wananchi.

Alisema anaamini mada walizofundishwa watumishi kuanzia ngazi ya vijiji hadi mkoa zitakuwa na tija kwao, hususani katika masuala haki na utawala bora, ambavyo ni msingi mzuri kwa kiongozi yoyote anayetekeleza majukumu yake ipasavyo.

Kutokana na hilo, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuzingatia yale watakayofundishwa na wataalamu kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, ili wakatumie kwa vitendo katika maeneo wanayotoka kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

Aliwasisitiza pia wazingatie kila mada itakayofundishwa ili na wao baada ya kumaliza mafunzo hayo wakaitoe elimu hiyo kwa wananchi wanaokuja kuhitaji msaada wa utafutaji haki katika vipengele tofauti.



# Bil.6/- zawaondoa katika umaskini wananchi 3,400

**Na Neema Emmanuel,**
ILEMELA

MRATIBU wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Manispaa ya Ilemela, Leonard Robert, amesema wananchi 3,450 kutoka kaya maskini wamenufaika na uwezeshwaji wa ruzuku ya zaidi ya Sh.bilioni sita katika kipindi cha miaka minne.

Alibainisha hayo juzi wakati wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kupitia mfuko huo katika manispaa hiyo na kueleza kuwa ruzuku hiyo imetolewa kuanzia Desemba 2020 hadi Desemba 2024.

Vilevile alisema ruzuku iliyotolewa kwa ajili ya uboreshaji wa miradi ya maendeleo tangu Desemba, 2021 hadi Desemba, 2024 imetekeleza miradi 46 ya zaidi ya Sh.bilioni 2.2 ambako miradi 33 imekamilika huku 13 ikiwa ipo katika utekelezaji.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani kutoka TASAF Dodoma, Uswege Edward alisema baada ya kuzungukia miradi hiyo walibaini kuwa imekidhi ubora na kuona thamani ya fedha iliyotolewa.

Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Mihama, Dk. Ng'hwaya Tenga, alisema zahanati hiyo ni moja ya miradi iliyotekelezwa kupitia TASAF ikigharibu Sh.milioni 241 na kusaidia kuokoa maisha ya wajawazito na kuwapunguzia adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya.

Alisema ujenzi wa zahanati hiyo ulianza mwaka 2022 hadi Mei 2024 na kwamba kabla ya zahanati hiyo wananchi walikuwa katika mazingira magumu ya upatikanaji wa huduma za afya, huku wengi walilazimika kujifungulia nyumbani.

Mkazi wa Mtaa wa Mihama, Agness Levocatus alisema mradi huo ni muhimu kwao kwa sababu walikuwa wanatembea umbali mrefu kufuata huduma za afya.

Alisema zahanati hiyo kwa sasa inatoa huduma na kuwanufaisha wananchi wa eneo hilo na walio jirani.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Shinyanga Mjini, Anord Makombe, akikata utepe kuzindua kituo cha bodaboda cha Majengo Mapya Sokoni juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Milioni 900/- zakarabati Hospitali ya Manispaa Geita

**Na Alphonce Kabilondo,**
GEITA

ZAIDI ya Sh. milioni 932 zimetumika katika ukarabati wa majengo katika Hospitali ya Manispaa ya Geita mkoani Geita, lengo likiwa ni kurejesha hadhi yake na kusaidia wagonjwa kupata huduma katika mazingira rafiki.

Mganga Mfawidhi wa Hosipitali hiyo, Dk. Thomas Mafuru, alisema hayo wakati akizunguma hospitalini hapo akisema fedha hizo zilizotolewa na serikali ili zimetumika katika kufanya ukarabati wa majengo mbalimbali muhimu.

Alitaja majengo hayo kuwa ni pamoja na chumba cha upasuaji, famasia, ujenzi wa wodi ya watoto njiti, wodi ya wazazi na wagonjwa wa nje, wodi ya wanawake na wanaume na chumba cha kuhifadhia maiti.

Mratibu wa Hospitali hiyo, Dk. Sospeter Marwa alisema fedha hizo zilipokelewa katika mwaka wa fedha 2023/24 na kutumika katika uboreshaji wa miundombinu ya hospitali hiyo.

Kadhalika, alisema sambamba na kuboreshewa miundombinu wameongezewa madaktari wenye shahada ya kwanza na kufanya hospitali hiyo kufikisha madaktari tisa ambao wanasaidia kuhudumia wagonjwa kwa wakati.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM Wilaya ya Geita, Robert Nyamaigoro, alisema hali ya hospitali hiyo kwa sasa inavutia tofauti na mwanzo.

"Madaktari hawa ni wazalendo mimi nimezaliwa hapa nafahamu miundombinu ya hospitali hii haikuwahi kuvutia hivi japo fedha zilikuwa zikitolewa lakini kwa maboresho haya tunasisitiza hata wagonjwa wahudumiwe ipasavyo," alisema Nyamaigoro.

Diwani wa Viti Maalumu wa Kalangalala, Zaituni Fundikira, alisema awali wananchi walikuwa wakihofia kuhifadhi miili katika hospitali hiyo kutokana na ubovu wa jokofu na hivyo kulazimika kuisafirisha kwenda Hospitali ya Sengerema mkoani Mwanza.

Alisema: "Kwa sasa jokofu la kisasa linauwezo wa kuhifadhi miili zaidi ya 10 kwa wakati mmoja ni maboresho ambayo yameondoa adha iliyokuwapo hapo awali".

## Ukarabati wa shule watajwa kumaliza tatizo la utoro

**Na Halima Ikunji,** KALIUA

ZAIDI ya Sh.milioni 500 zimetumika katika ujenzi wa mabweni manne pamoja na matundu ya vyoo 10 katika Shule ya Sekondari Mikindo iliyopo Kata ya Ichemba wilayani Kaliua mkoani Tabora.

Akizungumza na Nipashe shuleni hapo, Mkuu wa Shule hiyo, Annaemmy Mazigo, alisema uboreshaji wa miundombinu katika shule hiyo ikiwamo mabweni na vyoo kumesaidia kuongeza hali ya ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu na wanafunzi.

"Kujengwa kwa mabweni haya kumeleta hari na hamasa kubwa kwa watoto wa kike na kiume kupenda shule, hata utoro sasa umepungua sana na kila mtoto anasoma kwa bidii ili aweze kutimiza ndoto zake," alisema Mazigo.

Mkazi kutoka Mwongozo, Ashura Mohamed alisema kwa sasa tarafa hiyo imeboreshewa miundombinu hasa ya elimu hali inayosababisha kuwepo kwa ongezeko la wanafunzi shuleni.

"Vijiji na kata nyingi katika eneo hili havikuwa na shule za msingi wala sekondari lakini sasa shule zimejengwa katika kata na vijiji ambako mwaka wa fedha uliopita zilitolewa Sh.milioni 360 ili kujengwa Shule ya Msingi Langoni katika Kijiji cha Ibambo ili kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani," alisema Ashura.

Mbunge wa Jimbo hilo, Rehema Migira alisema kwa kipindi cha miaka minne ya Rais Samia kuwa madarakani kata zote 15 zimepata shule za sekondari.

Alisema pia shule za msingi zimeendelea kujengwa katika vijiji vyote ikiwemo kuboreshwa miundombinu ya shule zote.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Gerald Mongela alisema wakazi wa wilaya hiyo wanajivunia mambo makubwa yaliyofanywa na serikali hasa katika sekta ya elimu na kuboresha huduma za kijamii katika sekta zote.

Alibainisha kuwa shukrani za wana Kaliua zimeonekana kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka jana ambapo CCM ilipata ushindi wa asilimia 99 na kuahidi kuwa katika Uchaguzi Mkuu Rais Samia atapita kwa kishindo.

ama

ALHAMISI FEBRUARI 6, 2025

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

**Waziri Afya akiorodhesha uwekezaji mapinduzi afya kwa ubia na China**



Ukurasa 12

**AFYA YA AKILI...**

**Wataalamu na undani afya yake mama, mtoto inavyokuwa hatarini kwa sonona**

INA MARA MBILI YA WASTANI TAIFA...

# Wenye Shinyanga yao wafunguka kulikoni wanakuwamo 'nne bora ya malaria' kitaifa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UGONJWA wa malaria umekuwa tatizo kubwa katika maisha ya jamii, ukiambatana na madhara hadi hatua mbaya ya kifo.

Kitaaluma una kinga kadhaa, ikiwamo matumizi ya chandarua. Ni bahati mbaya kuna uelewa mdogo kwa wanajamii kuhusu kinga hiyo, umma ukiwa na mitazamo tofauti.

Wapo ambao wamekuwa wakituhumiwa na matumizi potofu ya vyandarua, katika ufugaji vifaranga vya kuku wasiweze kuliwa na kunguru na wanyama wengine.

Aidha, hiyo inatajwa kushamiri zaidi katika ukanda na mikoa yenye maziwa na mabwawa makubwa, nako kukitumika kuvulia samaki wadogo na hasa dagaa, sababu ikitajwa ni ukosefu wa elimu sahihi ya matumizi yake.

Baadhi yao hasa wanaoishi vijijini, pia wanatajwa kuhusisha malaria na imani za kishirikiana, wakielekeza tiba zao kwa waganga wa jadi.



Watu wakilala ndani ya vyandarua, mbinu mojawapo ya kukabili malaria. **PICHA: MTANDAO**

Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka jana, inakadiriwa watu milioni 263 wameugua malaria duniani, huku 597,000 walifariki katika nchi 83.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya WHO iliyotolewa Desemba mwaka jana, idadi hiyo ya maambukizi, inatajwa kuwa juu zaidi kwa maambukizi ya watu milioni 11 kulingana na mwaka 2022 na wastani wa vifo takriban vikifanana kwa miaka hiyo inayofuatana.

Hata hivyo, WHO inaonyesha tahadhari kwamba asilimia 95 ya vifo hivyo (wastani 567,150) vimetokea katika nchi za Kiafrika na idadi iliyobaki (wastani 29,850) ndio vinatokea katika mabara mengine duniani.

Pia, katika namna inayoonyesha malaria kuongezeka duniani, takwimu ya vifo duniani mwaka 2019 ilikuwa na maambukizi milioni 229 na vifo 409,000.

### HALI ILIVYO NCHINI

Takwimu za Kitaifa za Viashiria vya Malaria kwa Mwaka 2022 (Malaria Indicator Survey-2022), kiwango cha maambukizi ya malaria kitaifa ni asilimia 8.1%, mkoa Tabora ukiongoza kwa asilimia 23.4, ukifuatiwa na Mtwara (20%), Kagera (18%), kisha Shinyanga (16%), ambayo ni sawa ana asilimia 197.5 ya iliyopo kitaifa.

Kukabiliana nayo nchini, Wizara ya Afya imeibua mbinu mpya ya kugawa vyandarau bure kila kaya, kuhakikisha kasi yake inazuliwa kuwa tishio kwa umma.

Serikali pia, inaendelea kukabiliana na malaria kwa kunyunyizia dawa za kuua viluwiluwi vinavyosababisha ugonjwa huo kwenye makazi ya watu.

Vilevile kuna mwendelezo wa ugawaji vyandarua vyenye dawa na hasa kwa wajawazito kliniki, huku ikiendana na utoaji elimu kwa wananchi, namna ya kujikinga na kuua mazalia ya malaria.

### WIZARA AFYA/TAMISHEMI

Ofisa Mradi Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria kutoka Wizara ya Afya, Wilfred Mwafungo, anasema serikali kwa kushirikiana na wadau wake wa afya wanaendesha mbinu kadhaa.

Anataja kugawa chandarua bure kwa kila kaya, vikitolewa kupitia maofisa watendaji wa kata, vijiji na vitongoji na wale watakaobainika kuwauzia wafanyabiashara, wanachukulia hatua za kiutumishi, kwani inatajwa ni kuihujumu serikali katika mapambano yake.

Mwafungo anasema, utafiti uliofanyika umebaini, endapo mwananchi atatumia vema chandarua chenye dawa kulala ndani yake, ana nafasi ya kujikinga na ugonjwa kwa asilimia 63.

Anahimiza, kinachotakiwa kufanyika ni kuendeleza utoaji elimu kwa wananchi, kuhusu umuhimu wa matumizi sahihi ya chandarua, usafi wa mazingira na kuzuia maji kutuama, ili kuua mazalia ya mbu.

Vilevile ana angalizo akitaka kuhakikisha havitumiki kwa uvuaji samaki, kufuga kuku na bata au kuuzwa kwa wafanyabiashara.

Mdhibiti wa Wadudu Dhurufu kutoka Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Best Yoram, anasema, kuna vyandarua 1,542,836 vimetolewa mkoani Shinyanga na katika yake 841,503 (asilimia 54.54%) vitatolewa wilayani Kahama.

Hapo Yoram anatoa mchanganuo kwa halmashauri: Msalala itapata vyandarua 260,350; Ushetu 268,872; na Manispaa Kahama 312,836.

Anaeleza kitaifa, viashiria vya malaria mwaka 2022, kiwango cha maambukizi kilikuwa asilimia 8.1.

Yoram anawakumbusha wananchi kuacha kutumia dawa pasipo kupima na kujua anachoumwa, baadhi yao wamekuwa wakiumwa kichwa na kuhusisha na moja ya dalili ya ugonjwa wa malaria, huku wengine na hasa wanaoishi vijijini wakizama na mazoea kukimbilia tiba kwa waganga wa jadi, hali iliyo kinyume na kanuni za afya.

### KULIVYO KAHAMA

Mboni Mhita, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, anaeleza serikali imekuwa ikibuni mbinu za kukabiliana na ugonjwa huo, lakini inakwamishwa na wananchi kutozingatia maelekezo wanayopewa.

Inaendelea Uk. 13

AFYA YA AKILI...

# Wataalamu na undani afya yake mama, mtoto inavyokuwa hatarini kwa sonona

Na Christina Mwakangale

KADRI uzoefu wa mama aliyekwisha jifungua na hasa ambao kipindi cha ujauzito wamepitia changamoto kama vile uzazi pingamizi wakati wa kujifungua, huchangia kuwa na hofu ya uzazi ufuatao na hata kuathiri afya ya akili.

Mratibu wa Afya Akili na Utengamao wa Halmashauri ya Arusha, Dk. Paschal Kang'iria, anasema hali hiyo ndio ugonjwa wa akili unaoitwa sonona wakati wa ujauzito, huku hali hiyo ikimwathiri mama aliyetoka kujifungua.

"Mabadiliko ya homoni kipindi cha ujauzito na baada ya kujifungua ni jambo la kawaida, ingawa ugonjwa usipotibiwa, huwatetesha baadhi ya kinamama," anasema.

Dk. Kang'iria ametamka hayo mwishoni mwa wiki, wakati akitoa elimu kuhusu afya ya akili kipindi cha ujauzito na baada ya kujifungua. Kwamba hali ya tashwishi kwa mjamzito au aliyetoka kujifungua, husababisha utengamao duni kiakili.

"Afya ya akili naifananisha na barabara, asubuhi na jioni foleni ni kubwa, ndivyo ubongo unafanya kazi kwa vipindi tofauti," anaelimisha Dk. Kang'iria.

Ana ufafanuzi zaidi kwamba: "Barabara yenye msongamano barabarani, piga picha kichwani mwako pia unakuwa na msongamano wa mawazo. Afya ya akili huamua namna tunavyohisi, tabia zetu ni kama mwili ukiyumba ukachoka na akili inachoka pia.

"Ni afya ambayo inategemea namna unavyojifungamanisha na jamii. Mwingine timu yake ya mpira ikifungwa kesho akija ofisini anajisikia vibaya, anataniwa, anakuwa mnyonge hapa afya yake akili haiko sawa.

"Fikiria mama mwenye uzoefu wa kujifungua watoto wa jinsi moja, anawaza sijui nitapata tena mtoto wa sita wa kike? Mume wangu atanielewaje?

"Au mama kila anapojifungua anapitia uzazi pingamizi, anawaza safari hii nitajifungua kawaida au kwa upasuaji? Hofu, wasiwasi, maumivu ya 'labour' (chumba cha kujifungua), hasa kwa ambao ni uzazi wa kwanza. Hali hizo zikidumu, afya ya akili inayumba."

Anasema changamoto iliyoko hivi sasa, hata kukuza magonjwa ya akili kama vile sonona, msongo wa mawazo kwa kundi hilo, ni kukosa uhusiano wa karibu na familia, wenza au jamii.

"Wanandoa au wenye uhusiano, hata 'single mother' (mama asiyeolewa), ana ujauzito, baba hamwoni, hata walio kwenye ndoa baadhi ndoa haijatulia mawazo muda wote, mama huyu huathiri afya ya akili," anaongeza Dk. Kang'iria.



Mtaalamu wa afya na Mratibu wa Afya ya Akili na Utengamao wa Halmashauri ya Arusha, Dk. Paschal akitoa elimu kwa wanafunzi namna ya kujihadhari na maradhi ya sonona. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

> **"Homoni ya mapenzi ikiachiliwa inaweka 'bond' ya mapenzi kati ya mama na mtoto aliyeko tumboni na mama. Ingawa mama akiwa mjamzito si kwa kupenda kwake, bali kile alichokuwa anakiwaza, akaingia katika sonona, muunganiko wao utapotea.**

**MSAIKOLOJIA TIBA**

Msaikolojia Tiba kutoka Hospitali ya Saifee, Dar es Salaam, Sifa Hyera, anasema athari za sonona kipindi cha ujamzito na baada ya mama kujifungua, zisipotibiwa mapema, humwathiri mtoto aliyeko tumboni na akishazaliwa humsababisha kuwa na uhusiano duni kijamii.

Katika tamko lake mwishoni mwa wiki kwenye mjadala wa elimu ya afya ya akili kwa mama, Sifa anaungana na mtaalamu mwenzake, akisisitiza umuhimu wake, kabla na baada ya kujifungua; kupunguza madhara ya sonona.

Ni mjadala ulioandaliwa na Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe (MNH), Sifa, akiitambulisha sonona kwa mjamzito, inavunja anachokitaja kitaalamu 'bond' (nguzo) ya mapenzi kati ya mama na mtoto.

"'Bond' ni muunganiko wa kihisia na kimwili, ambao huanza wakati wa ujauzito na kuendelea katika maisha ya mtoto.

"Mabadiliko ya homoni ni kawaida kwa mjamzito, lakini ikisababisha sonona humwathiri mtoto, ila hutibiwa kisaikolojia au dawa," anasema.

Mtaalamu huyo anasema magonjwa ya akili yapo aina nyingi, ikiwamo sonona, inayohusiana na hisia na hutafsiriwa kwa dalili kama endelevu ya huzuni, kupoteza hamu, pia hasira.

"Sonona huonekana kwa dalili tofauti kwa kipindi cha wiki mbili, kwa mgonjwa kukata tamaa, kukosa usingizi au kulala kupitiliza, kushtuka usingizini, kula zaidi au kula kidogo," anaeleza.

Pia, anataja vyanzo vya sonona viko vingi, ikiwamo katika vinasaba ndani ya ukoo au familia kurithishana.

Kadhalika, msaikolojia tiba huyo, anasema hali alizokutana nazo mara kadhaa kwenye taaluma yake, nyingi amebaini wanaougua, chanzo ni kutokana na ugomvi kati ya mtu au jamii inayomzunguka kwa muda mrefu.



Mtu anayeonekana katika lindi la mawazo. **PICHA: MTANDAO.**

"Sonona inatibika, mojawapo ni kwa kutumia dawa na nyingine ni ya 'saikotherapi' (tiba saikolojia) kutoka kwa wasaikolojia tiba.

"Sonona kwa mjamzito, dalili hufanana na sonona za kawaida, mtu kupoteza 'interest' (mapenzi)... kuwa na huzuni kupitiliza, hamu ya kula haipo, kapungua au kuongezeka uzito.

"Au mama anakuwa na hofu, hasa akihofia muda wa kujifungua atakapokuwa 'labour'. Mtu akiwa mjamzito kuna kuwa na homoni huwa zinaongezeka na kusababisha mabadiliko ya kihisia.

"Kwa ambaye hajaolewa au uhusiano haueleweki, anaweza kujikuta kwenye sonona ya kipindi cha ujauzito," anasema mtaalamu Hyera.

Pia, anaeleza kuwapo athari kwa mtoto, iwapo mjamzito atakawa na sonona, anakuwa hatarini kuzaliwa njiti, au kutokuwa sahihi na akawa anabadili hatua za ukuaji taratibu sana.

"Homoni ya mapenzi ikiachiliwa inaweka 'bond' ya mapenzi kati ya mama na mtoto aliyeko tumboni na mama. Ingawa mama akiwa mjamzito si kwa kupenda kwake, bali kile alichokuwa anakiwaza, akaingia katika sonona, muunganiko wao utapotea.

"Matokeo ya sonona kwa mjamzito ni mtoto atakayezaliwa kuwa na hasira, kukosa upendo, kuhusiana na watu akikua. Mtoto huyo pia anaweza akaja kupata magonjwa ya akili hapo baadaye akikua.

"Si watoto wote wanaozaliwa na kinamama waliopitia sonona wakawa na matatizo hayo, lakini inaweza kuchangia matokeo hayo kwa mtoto kwa kiwango kikubwa.

"Asilimia 60 ya wajawazito wanapitia sonona duniani, lakini inatibika, iwapo utafika kupata matibabu mapema, ili kupunguza athari hasi kwa mtoto kabla ya kuzaliwa," anasema.

**BAADA KUJIFUNGUA**

Sifa anasema kwamba, mmoja kati ya kinamama saba, huweza kuwa na sonona baada ya kujifungua na dalili kuwa ni zilezile, kama; hasira, kujiona hawafai hata kuwaza kujidhuru au kumdhuru mtoto uliyemzaa.

"Mama akishajifungua hubadili ratiba, kulala, kuamka, hivyo kama hakujiandaa, anaweza kupata sonona. Nakumbuka Muhimbili (MNH), kulikuwa na 'kesi' mama aliyejifungua akapata sonona na kuanza kumdhuru mtoto.

"Tatizo kuu ni changamoto kwa mtoto kukosa kujenga muunganiko kwa jamii, hana uhusiano wa kijamii, anachelewa kukua na atasumbuliwa na vingi," anahitimisha.

AFYA

# Waziri Afya akiorodhesha uwekezaji mapinduzi afya kwa ubia na China

**Na Yasmine Protace**

SERIKALI kupitia Wizara ya Afya, imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya afya, huku katika sura ya pili taifa rafiki la China, likiendeleza uwekezaji kitaaluma na vifaa.

Lengo ni kufanyika uwekezaji mkubwa katika fani hiyo, kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya, ikithibitishwa na waziri mwenye dhamana, Jenista Mhagama.

Anasema, serikali kupitia Wizara ya Afya, imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika Sekta ya Afya, kukabiliana na vifo vitokanavyo na magonjwa ya moyo.

Waziri Mhagama anasema kuwa, takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) za mwaka 2019, zinaonyesha kuwa takribani watu milioni 17.9 hupoteza maisha kila mwaka, kutokana na magonjwa ya moyo, ikiwa sawa na asilimia 32 ya vifo vyote.

Ni tamko lake Waziri Mhagama, kwenye uzinduzi wa Kliniki ya Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), iliyopo Oyster Bay, Dar es Salaam.

"Kati ya vifo hivi, asilimia 85 husababishwa na mshtuko wa moyo pamoja na kiharusi. Takwimu hizi zinaonyesha ukubwa wa tatizo la magonjwa haya duniani na Tanzania ikiwamo," anaeleza.

Waziri anasema, kutokana na changamoto hiyo kubwa duniani, serikali chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ikafanya uwekezaji mkubwa kwa kiwango cha kimataifa, kwenye vifaa tiba pamoja na mitambo, zikiwamo mashine za uchunguzi wa magonjwa kama; MRI, CT- Scan na Ultrasound.

"Katika taasisi hii ya JKCI, Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amewezesha usimikwaji wa mashine tatu za 'Cathlab carto' kwa ajili ya upasuaji kwa njia ya tundu dogo.

"Upasuaji huu umepunguza kwa kiwango kikubwa muda wa mgonjwa kukaa hospitali," anasema Waziri Mhagama.

Anafafanua kuwa, serikali inaendelea kuhakikisha hospitali zinakuwa na uwezo wa kutoa huduma za matibabu kwa wananchi katika namna mbalimbali, ikiwamo programu ya tiba mkoba (Outreach Programme) ijulikanayo kwa jina la 'Dk. Samia Suluhu Hassan Outreach Programme.'

"Upanuzi wa huduma za kibingwa za matibabu ya magonjwa ya moyo katika hospitali zetu za kanda; Chato, Hospitali ya Benjamin Mkapa, Hospitali ya Kanda Mtwara na nyinginezo, umeonyesha dhamira ya dhati na kutafsiri kwa vitendo dhana ya Utalii Tiba, watu kutoka mataifa mengine kuja kutibiwa nchini," anasema.

Pia, Waziri Mhagama anaeleza mkakati wa 'Bima ya Afya Kwa Wote' unaendelea, akiahidi utakuwa mworobaini wa changamoto nyingi za upatikanaji huduma za afya nchini.

Hapo anahimiza: "Kwa pamoja tuungane katika kuwaelimisha wananchi umuhimu wa 'Bima ya Afya kwa Wote' kuwa ndio mkombozi wa huduma za matibabu kwa Watanzania," anasema Waziri Mhagama.



Waziri wa Afya, Jenista Mhagama katika tukio la kupokea msaada wa vifaa tiba kutoka China, vyenye thamani ya Shilingi milioni 125, vilivyokabidhiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam Januari 24, 2025. **PICHA: MAKTABA**

**MKUU JKCI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Peter Kisenge, anasema taasisi hiyo kwa sasa inaweza kuwaona wagonjwa hadi 300 wa upasuaji wa tundu na wagonjwa 800 wa upasuaji wa kifua kwa siku.

Anaeleza kwamba wamejiwekea malengo ya kuwaona wagonjwa 3,500 wa upasuaji wa tundu kwa mwaka, pia wagonjwa 900 wa upasuaji wa kifua kwa mwaka.

**MSAADA SH. MILIONI 125**

Serikali ya China katika kuiunga mkono Tanzania, imeipatia vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 125 vilivyokabidhiwa kwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dar es Salaam.

Inatajwa, kuwa sehemu ya utekelezaji wa makubaliano kati ya Tanzania na China, huku Waziri wa Afya, wakati akipokea vifaa hivyo, anautaja kuwa ushahidi wa mshikamano imara na utayari wa mataifa hayo kwa pamoja kuimarisha huduma za afya nchini.

"Msaada huu ni mchango muhimu sana katika kukabiliana na mahitaji ya huduma za afya kwa wananchi, pia katika kuimarisha ushirikiano na urafiki kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China," anasema.

Waziri Mhagama anautaka uongozi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, kuvitunza vifaa hivyo na kuvihudumia kwa wakati inapobidi, vitumike muda mrefu, kuimarisha utoaji huduma wenye matokeo chanya kwa umma.

Waziri Mhagama anasema, serikali ya China imeendelea kutuma timu ya wataalamu wa afya nchini kila baada ya miaka miwili.

Anataja kwamba imekuwa mkubwa kwa hospitali nchini, kupitia mafunzo wanayotoa kwa wataalamu wa ndani zikiwa za ngazi za ubingwa na ubobezi.

Balozi wa China nchini, Chen Ming Jian, anasema nchi yao itaendelea kushirikiana na Tanzania kuboresha huduma za afya kwa wananchi, ikiwamo katika vifaa tiba, akitaja ushirikiano huo una zaidi ya miaka 60.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Prof. Mohamed Janabi, anaishukuru Wizara ya Afya kudumisha ushirikiano wake na China, akitamka " ushirikiano huu unamanufaa makubwa sana Tanzania hasa katika sekta ya afya.

# Wenye Shinyanga yao wafunguka kulikoni wanakuwamo 'nne bora ya malaria' kitaifa

**INATOKA UK. 11**

Hapo anawanyooshea vidole maofisa watendaji wa kata na vijiji, wanaotuhumiwa kuuza chandarua kwa wafanyabiashara.

Mkuu wa Wilaya - Mhita, anatamka kashfa zao, kwamba awali waliwadanganya wananchi kwamba vyandarua vimeisha, hata wakakwamisha mapambano hayo ya malaria.

Kidole chake cha ukali akakifikisha pia kwa wafanyabiashara wanunuzi wa vyandarua vya wizi, akinena hatua za kisheria, ikiwamo kufikishwa mahakamani kwa dai la kuhujumu serikali, akitaja wilayani kwake vimetengewa vyandarua 841,503.

**VIONGOZI WA DINI**

Alhaji Omari Damka, Shekhe wa Wilaya ya Kahama, anasema, elimu inahitajika kuendelea kutolewa kwa wananchi, kuhusu matumizi sahihi ya vyandarua na uuaji wa mazalia ya mbu.

Anasema, katika msimu uliopo wa kilimo, pia mjumuiko wa wakulima kupitia vyama vyao, itumike kuwafikishia elimu na mgawo wa vyandarua, huku yeye akitumia kuwasilisha hilo muda wa ibada.

Mchungaji wa Kanisa la Anglikana, Emmanuel Maziku, anamuuga mkono akisema elimu ya matumizi ya chandarua kutibu malaria kwa wananchi hasa wa vijijini, imesahaulika kulinganisha na maradhi mengine.

Anashauri umma vijijini watembelewe, wakipatiwa elimu ya kujikinga na ugonjwa huo unaozuilika, kupitia chandarua chenye dawa.

Maziku kama alivyo mtangulizi wake mdhamini wa kiimani, anaahidi kutumia nafasi yake kufikisha darasa la malaria na umuhimu wa chandarua katika ibada zake.

Mchungaji Maziku ana maelezo: "Kipindi cha ugonjwa wa Uviko-19, tulishirikiana na wataalamu wa afya kila kona na tukahamasishana namna ya kujikinga kwa kuvaa barakoa na kunawa mikono wakati wote na tulifanikiwa.

Anaendelea: "Na hili suala la ugonjwa wa malaria, tunaweza kulidhibiti kama tutakuwa na ushirikiano wa kutoa elimu juu ya matumizi ya chandarua... nawaahidi somo hili litakuwa moja ya mada zangu kila siku kanisani."

**SAUTI YA WAKAZI**

Mkazi wa Mtaa wa Masaki, Kata ya Malunga, Manispaa ya Kahama Shukrathi Juma, anasema wengi wao hawana elimu sahihi ya utumiaji chandarua na wamekuwa wakitumia kipindi cha ujauzito wao kwa maelekezo ya kiliniki.

Anakiri kuwapo wenzao kinamama, wanapopewa vyandarua kliniki, huishia kuwekewa uvunguni mwa vitanda majumbani, akiainisha sababu ni dunia na wapo wanaotumia kufugia kuku na bata.

Greyson Dotto, anayeishi Kata ya Nyasubi, Kahama, anasema mikoa yenye shughuli za uvuvi ameshuhudia wavuvi wakitumia vyandarua kuvua dagaa, akitaka nao wakaelimishwe undani wa mapambano ya malaria.

Anasema, hata yeye awali hakuona umuhimu wa chandarua, mpaka pale alipougua na kulazwa hospitalini kwa wiki mbili, vilevile mkewe akapata darasa kama hilo kliiniki, alipokuwa mjamzito.

"Kwa sasa, nikiumwa malaria sio kwa sababu ya kutotumia chandarua (neti) bali nitakuwa nimeipata wakati wa kutizama televisheni na familia yangu.

"Muda wa kulala nahakikisha wote wako kwenye chandarau na wanaolala bila chandarua huwa nawapatia adhabu..." anasema Dotto.

KILIO MAJI MACHAFU...

# Mganga Mkuu, bosi RUWASA, DC na ufafanuzi maji wakazi kudhurika

**Na Christina Haule, aliyekuwa Kilosa**

***ALHAMISI wiki mbili zilizopita, safu hii ilikuwa na sehemu ya kwanza iliyofafanua hali ngumu ya upatikanaji maji wilayani Kilosa, mkoani Morogoro. Endelea nayo, kwa ufafanuzi wa mamlaka zinazosimamia maji na afya, pia hatua zijazo kutatua changamoto hiyo.:***

KUNA madai wilayani Msowero, kwamba, hali ya utekelezaji usioridhisha wa Sheria ya Maji ya Mwaka 2019, umesababisha Kata ya Msowero kutoingizwa kwenye Bajeti za Maji katika miaka ya fedha, 2023/24 na 2024/25.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Kilosa, Mhandisi Sylvia Ndimbo, anakiri kata ya Msowero yenye vijiji vinne – Msowero, Mambegwa, Mkogwe na Majambaa, bado havijaingizwa kwenye bajeti hiyo za maji.

Uhalisia wake unatajwa kuchangia kuwapo changamoto ya maji kwa zaidi ya miaka 10 mahali hapo, kukiwapo athari mbaya za matukio ya vifo na kulazwa kwa watu 20 kutokana na magonjwa ya matumbo yakiripotiwa katika mwaka 2024.

Mhandisi huyo anasema, kutoingizwa kwenye bajeti, kunasababishwa na ukomo wa bajeti zinazopangwa kila mwaka, ambazo hazitoshelezi kufikia kata na vijiji vyote kwa wakati mmoja.

Mhandisi Sylvia anabainisha kuwa, katika wilaya ya Kilosa yenye vijiji 138, kuna vijiji 23 havina kabisa huduma ya maji safi na salama.

Anataja suluhisho lake, ni kwamba RUWASA ina mpango wa kupeleka maji kwa vijiji hivyo kwa hatua, kwa kuzingatia uwezo wa bajeti ya kila mwaka.

"Kwa mfano, ujenzi wa kisima kimoja hugharimu takriban shilingi milioni 30 na kwa bajeti ya mwaka, tunaweza kujenga visima 10 au 12 pekee," anasema Mhandisi Sylvia.



Kaimu Meneja wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Kilosa, Mhandisi Silvia Ndimbo (kushoto), akitoa maelekezo ya ujenzi wa tangi la maji kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi vijijini. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE**

> **"Sababu mtu anaweza kutumia moto uleule anaopikia chakula jioni na baadaye kubandika maji kwenye moto huo na asubuhi yanakuwa yameiva.**



Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Kilosa, Dk. Selemani Kasuguru akifafanua jambo kuhusu hali ya shida ya maji wilayani humo, ikisababisha magonjwa.

### CHANGAMOTO ZA MIUNDOMBINU

Mhandisi Ndimbo, anasema RUWASA hufikisha huduma kwenye taasisi za huduma za kijamii, kama zahanati na shule, kulingana na bajeti zilizopo.

Hata hivyo, jukumu la kuingiza maji ndani ya taasisi hizo ni la halmashauri za wilaya.

Mhandisi Sylvia anasema, kwa sasa wanajipanga kutembelea Kata ya Msowero, ili kuwasaidia wakazi wa vijiji na vitongoji vilivyokosa maji, kama A-Mzanini na Sekondari ya Msowero, Kijiji cha Majambaa, kwa kuwachimbia visima vifupi.

Mkurugenzi wa wakati huo wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, Michael Gwimile, anasisitiza umuhimu wa RUWASA kuanza taratibu za kuweka miundombinu ya maji mara ujenzi wa maeneo yenye miradi ya kijamii unapoanza.

"Hii itasaidia kupunguza changamoto za maji na kuimarisha huduma za kijamii," anasema Gwimile, akiongeza: "mfano kijiji kuna ujenzi wa zahanati na kama RUWASA wakiweka huduma za maji mapema itasaidia kufikisha huduma hiyo kwa jamii."

"Pia, hata kama bajeti hazijakaa sawa, watakuwa wamepata huduma na kupunguza malalamiko," anasema Gwimile.

Anafafanua kuwa, halmashauri nazo hulazimika kuchimba visima vifupi na virefu, baada ya miradi mbalimbali ya kijamii kukamilika, katika baadhi ya maeneo, ili kukabiliana na changamoto za maji.

### ATHARI ZAKE

Ofisa Mtendaji Kata ya Msowero, Mustafa Sadi, anasema changamoto za maji zimeathiri wakazi wapatao 30,674 (kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022).

Vijiji kama Mambegwa vina bomba moja pekee, ambalo pia ni bovu, tangu mwaka 2019, taasisi isiyo ya kiserikali ya Waridi, ilisaidia kupunguza changamoto za maji kwa kuchimba visima viwili.

Inatajwa, mafuriko ya mwaka 2024 yalirejesha hali mbaya kwa kusababisha vifo na magonjwa ya matumbo kwa wakazi.

Anavitaja vijiji na vitongoji vilivyokosa maji katika Kata ya Msowero kuwa baadhi ya vitongoji kwenye kijiji cha Msowero, kijiji cha Majambaa, kijiji cha Mkogwe na Mambegwa, ambacho kina bomba moja la Mdundiko, nalo ni bovu.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Kilosa, Dk. Selemani Kasuguru, anasema, wagonjwa wa matumbo na kuhara, zaidi inatokana na matumizi ya maji yasiyo safi na salama.

Dk. Kasuguru anasema, licha ya idadi ya wagonjwa kushuka kutoka 3,815 mwaka 2022/23 hadi 2,934 mwaka 2023/24, anakiri tatizo bado kubwa.

Hivyo Dk. Kasuguru anahimiza wakazi kutumia dawa za kusafisha maji na kuchemsha maji ya kunywa, ingawa wengi wanaogopa gharama.

Anasema wamekuwa wakiwaelimisha wakazi juu ya matumizi ya dawa za kidonge za kusafisha maji au kuchemsha maji ya kunywa lakini wakazi wengi wamekuwa wakishindwa kufuatilia elimu hiyo, kwa sababu ambazo hazina ukweli ikiwamo kuwa hawana uwezo wa kununua mkaa kwa ajili ya kuchemshia maji ya kunywa.

"Eti wanaogopa gharama, mbona hakuna gharama! Ni rahisi kuchemsha maji na kupata majisafi na salama ya kunywa kwa kila mtu.

"Sababu mtu anaweza kutumia moto uleule anaopikia chakula jioni na baadaye kubandika maji kwenye moto huo na asubuhi yanakuwa yameiva," anasisitiza daktari huyo wa wilaya.

Dk. Kasuguru anasema, Sheria ya Maji, pia Sera ya Maji ya mwaka 2002 zinahitaji kuimarishwa katika utekelezaji.

Hapo anasisitiza RUWASA inapaswa kuhakikisha mifumo ya usambazaji maji safi na salama inaboreshwa, ili kuzuia magonjwa ya milipuko.

Shirika la Afya Duniani (WHO) nalo limeonya kuwa ongezeko la magonjwa ya kipindupindu duniani, linahitaji hatua za dharura katika upatikanaji maji safi na salama.



## Mwigulu: Tusigawanyike, tusitoane macho kisa uchaguzi

**Na Thobias MWanakatwe,** IRAMBA

MBUNGE wa Iramba Magharibi, Dk.Mwigulu Nchemba, amewataka wanachama wa CCM kutokuwa na sababu ya kugawanyika na kutoana macho kwa ajili ya uchaguzi, badala yake wabakie kushughulika na agenda moja tu ambayo ni maendeleo.

Alisema hayo jana wakati wa maadhimisho ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutimiza miaka 48 tangu kianzishwe yaliyofanyika kiwilaya katika Kata ya Kyengege wilayani Iramba mkoani Singida

"Hatupaswi kugawanyika eti tunawaza uchaguzi kwasababu kitu kimoja ambacho huwa inakuwa ni agenda ni mambo ya maendeleo, kama umepata maendeleo kwanini mnataka kutoana macho kwa ajili ya uchaguzi," alisema.

Dk.Mwigulu alisema hivi sasa kilichosalia ni kuangalia mwaka 2025 kwenda 2mwaka 030 kwani kazi kubwa ya kuleta maendeleo nchini iliyofanywa na serikali ya CCM inakifanya chama kionekane kipo sehemu sahihi.

"CCM ni chama ambacho kinaaminiwa na Watanzania ndiyo maana kinaendelea kupewa dhamana ya kuongoza nchi kwani ni chama kilichojenga umoja wa nchi hii ni chama kilichojenga mshikamano ni chama kilichoimarisha undugu wa Watanzania," alisema.

Alisema kutokana uimara ya CCM ndiyo maana Tanzania imekuwa taifa linalopigiwa mfano na mataifa mengine kutokana na utamaduni na undugu mzuri uliojengwa tangu kuasisiwa kwa taifa hili na uongozi bora unaotolewa.

"Utaratibu mzuri wa kupata viongozi umeifanya Tanzania kuwa ni taifa ambalo linaendelea kuheshimika duniani kote ambalo linategemewa na nchi nyingi za Afrika na limekuwa ni kisiwa cha amani kimbilio la wengi," alisema.

Dk. Mwigulu alisema watu wasichukulie poa tu CCM ni chama chenye heshima akisema ndiyo maana mtu hawezi kuiongelea CCM bila kuiongelea Tanzania.

# Sensa ya Uzalishaji Viwandani kuanza mwezi ujao

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kufanya sensa ya uzalishaji viwandani kwa muda wa miezi mitatu, kuanzia Machi mwaka huu, itakuwa ya kwanza kuhusisha pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Selemani Jafo, alisema hayo juzi jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu sensa hiyo ya uzalishaji viwandani.

Alisema lengo la sensa hiyo ni kupata taarifa za kina za kitakwimu zitakazo iwezesha serikali na wadau kufanya maamuzi yenye ushahidi wa kitakwimu katika kuhuisha na kuboresha sera, mipango na programu za maendeleo ya sekta ya viwanda na uchumi wa kitaifa kwa ujumla.

"Aidha matokeo haya yatatumika kupima utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, program za kikanda kama vile Dira ya Afrika Mashariki 2050, Agenda ya Maendeleo ya Afrika 2063," alisema.

Alisema: "Malengo Endelevu ya Dunia 2030 (SDGs) hususani lengo namba sita kuhusu upatikanaji wa maji safi na salama, lengo namba saba kuhusu upatikanaji wa nishati safi na ya gharama nafuu na lengo namba tisa kuhusu maendeleo ya viwanda, ubunifu na miundombinu"

Vilevile, alisema sensa hiyo itakusanya taarifa kutoka viwanda vyenye wafanyakazi kuanzia 10 au zaidi na kundi la viwanda vyenye wafanyakazi kuanzia mmoja hadi tisa.

Alisema kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi kwa viwanda vidogo zitafanyika kwa sampuli kutokana na wingi wa viwanda na sifa zinazofanana.

Pia, alitoa wito kwa wadau wote katika sekta ya viwanda nchini kushirikiana na serikali kufanikisha utekelezaji wa sensa hiyo ya uzalishaji viwandani.

Alisema: "Nitoe wito kwa wadau mbalimbali katika sekta ya viwanda nchini kutoa ushirikiano katika kufanikisha utekelezaji wa sensa hii kwani kwa atakaye ficha taarifa zinazohitajika atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria zilizopo".

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema sensa hiyo inatarajiwa kufanyika kwa muda wa miezi mitatu kuanzia Machi hadi Juni mwaka huu ambapo majibu yatatolewa.

Tanzania Bara, ilifanya sensa za uzalishaji viwandani mwaka 1963, 1978, 1989 na 2013 na kwa upande wa Zanzibar zilifanyika mwaka 1989, 2002, 2008 na 2012.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, mkoani Singida, James Mkwega (mbele), akiwaongoza wajumbe wa Kamati ya Mipango, Fedha na Utawala ya halmashauri hiyo, walipotembelea kukagua ujenzi wa Shule ya Sekondari Kidarafa, kata ya Mwanga, wilayani humo, juzi. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Tanzania, Norway zasaini mkataba kuwasaidia wakulima

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TANZANIA imesaini mkataba wa miaka mitatu na Serikali ya Norway kupitia taasisi zinazosimamia kilimo nchini wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 1.3 kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wadogo kujikwamua na changamoto zinazowakabili kwenye sekta hiyo.

Mkataba huo umesainiwa kupitia taasisi zinazosimamia kilimo nchini ambazo ni AGCOT, AGRA na ATO.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde akizungumza katika hafla hiyo jana jijini hapa, alisema lengo la mkataba huo ni kuhimiza kilimo kinachozingatia hali ya mazingira ya sasa ikiwemo kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Alitaja lengo lingine ni kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao, kuinua uchumi wa wakulima wadogo, pamoja na kuimarisha usalama wa chakula nchini.

"Tunaipongeza sana Serikali ya Norway kutokana na kutoa fedha hizo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo wa kilimo, tutaendelea kushirikiana nao kuhakikisha sekta ya kilimo inazidi kukua hapa nchini," alisema Silinde.

Aidha, alisema kusainiwa kwa mkataba huo kutasaidia pia kufungua vizuizi vya udhibiti wa kilimo, kufungua mipaka ya masoko ya nje ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi kwenye kilimo, kitendo kitachosaidia kuzidi kutanua wigo wa wakulima kuendesha kilimo chenye tija.

"Mkataba huu utasaidia wakulima wadogo wa ndani kuongeza uzalishaji katika kilimo cha mazao mbalimbali, lakini wapige hatua moja kwenda nyingine ili waweze kukua zaidi kiuchumi ikiwemo kuzifikia fursa mbalimbali za masoko ili kukidhi mahitaji husika," alisema

Balozi wa Norway nchini Tanzania, Tone Tinnes, alisema serikali yake itaendelea kushirikiana na Tanzania katika sekta ya kilimo ili kuhakikisha uchumi wa nchi unakua lakini pia wanaimarisha usalama wa chakula.

Alisema kwa zaidi ya miaka 60 nchi hizo zinauhusiano mzuri katika sekta ya kilimo ambapo alisema ushirikiano huo utazidi kuimarika.

Alisema: "Naipongeza Serikali ya Tanzania kuwekeza katika sekta ya kilimo, hii itazidi kuinua wakulima wadogo kiuchumi ili kuzifikia fursa zinazotolewa na serikali".



# Jela maisha kwa kumnajisi mtoto wa miaka mitano

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKAZI wa Kijiji cha Ibale Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, Casto Mwakalinga (20), amehukumiwa kifungo cha maisha jela kwa tuhuma za kumnajisi mtoto wa miaka mitano ambaye jina lake limehifadhiwa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga aliyasema hayo alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu mafanikio ya operesheni mbalimbali za jeshi hilo.

Alisema kijana huyo alihukumiwa Januari 28 mwaka huu na Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Kyela, Paul Barnaba ambaye ndiye aliyekuwa anasikiliza kesi hiyo kwa kushirikiana na Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Bihemo Mayengela.

Alisema wakati wa kutoa hukumu hiyo, Hakimu Barnabas alisema mshtakiwa alitenda kosa ambalo ni kinyume cha Kifungu cha 130 Kifungu kidogo cha kwanza na cha pili (e) na Kifungu cha 131 Kifungu kidogo cha kwanza vyote vya Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2022.

Alisema mshtakiwa alitenda kitendo hicho Oktoba 29, 2024 baada ya kumkuta mtoto huyo akiwa na mwenzake wanaangua maembe na ndipo akaungana nao kuangua matunda hayo na kwamba watoto hawakumwogopa kwa sababu walikuwa wanamfahamu.

Alisema mtuhumiwa alimkamata mtoto huyo na kuingia naye kwenye migomba kisha kuanza kumnajisi huku akimtishia kuwa angemuua endapo angesema kwa mtu yeyote.

"Alikuwa amejenga mazoea na watoto hao ili wasiogope kucheza naye, lakini baada ya kumkamata mwathirika na kuingia naye kwenye migomba alimtishia kuwa atamuua akisema," alisema Kamanda Kuzaga.

Aliwataka wazazi na walezi kuwa makini na watu wazima wanaojenga mazoea na watu wasiowafahamu akidai kuwa baadhi yao huwa wanakuwa na nia ovu.

Vilevile, aliitaka jamii kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo pindi yanapotokea matukio ambayo ni mabaya ili washirikiane kuyatokomeza na kuifanya jamii kuishi maisha ambayo hayana migogoro.

Katika hatua nyingine Kamanda Kuzaga alisema jeshi hilo kwa kushirikiana na askari wa wanyamapori waliwakamata watu wanne wakazi wa Wilaya ya Mbarali kwa tuhuma za kukutwa na nyara za serikali ambazo ni vipande viwili vya meno ya tembo.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Dadrahimu Aladad (74) mkazi wa Igalako, Daud Masengwa (55) mkazi wa Mahango Ruiwa, Mkombe Mathias (34) mkazi wa Mwatenga na Dotto Daimon (39) wote wakazi wa Mwatenga.

Alisema watuhumiwa walikutwa wakiwa na jino moja zima na vipande viwili vya meno ya tembo katika mfuko wa sandarusi wakiwa wamefícha nyumbani kwa mtuhumiwa Dadrahimu wakitafuta mteja wa kumuuzia.

Alisema watuhumiwa hao ni wawindaji haramu wa wanyamapori katika maeneo mbalimbali ya hifadhi za taifa ikiwamo Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ambayo iko jirani na maeneo ya makazi yao.

Vilevile alisema jeshi hilo linawashikilia watu watatu ambao ni Faraja Majengo (19) mkazi wa Kijiji cha Majengo wilayani Chunya, Fidelis Mdutu (25) na Charles Mfilinge (39) wote wakazi wa Iyowanza wilayani Mbarali kwa tuhuma za kupatikana na bunduki mbili aina ya gobole bila kuwa na kibali cha kumiliki silaha hizo.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa njiani na askari waliokuwa doria katika Kijiji cha Majengo na Kijiji cha Iwalanje na walipofanyiwa upekuzi walikutwa na silaha hizo pamoja na goroli 228 ambazo huzitumia kama risasi katika silaha hizo, mafataki 14, vipande 16 vya nondo na unga wa baruti makopo mawili.

Alisema mmoja wa watuhumiwa hao alikutwa na nyara za serikali ambazo ni nyama ya swala bila uwa na kibali hali ambayo inaashiria kuwa watuhumiwa ni wawindaji haramu wa wanyamarori kwenye hifadhi za taifa.



Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Warwick cha Uingereza, William Mwinuka (kushoto), akifundisha kuhusu matumizi ya lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia kwa walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati kutoka mikoa ya Songwe, Rukwa na Katavi, wanaopata mafunzo endelevu ya walimu kazini kupitia Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari nchini (SEQUIP), katika Sekondari ya Wasichana Mpanda, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Halmashauri ya Njombe yakusanya bil. 4/- 2024/25

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

HALMASHAURI ya Mji wa Njombe imevuka malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa zaidi ya asilimia 11 baada ya kukusanya Sh. bilioni 4.2 ambayo ni sawa na asilimia 61 kati ya 50 ambayo ilipaswa kukusanywa katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/25.

Hayo yalibainishwa juzi wakati wa kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji Njombe kilichofanyika mjini hapa.

Akiwasilisha taarifa ya halmashauri kuhusu mapato yaliyopatikana katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/25, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Njombe, Erasto Mpete alisema kuanzia Julai hadi Desemba 2024 ilikusanywa Sh. bilioni 4.209 sawa na asilimia 61.

"Natumia fursa hii kuwapongeza sana kwa sababu hii ni ishara ya ushirikiano pamoja na kamati ya fedha madiwani wote pamoja na wananchi ulituwezesha kufikia asilimia hizi," alisema Mpete.

Mpete alisema kwa upande wa taarifa ya hali ya usafi na kampeni yake ilivyofanikiwa huku akiwataka madiwani kuwa mstari wa mbele katika shughuli zote zinazolenga kuifanya halmashauri kuwa mfano wa kuigwa katika mambo yote.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Nganyagwa Erneo, alisema licha ya mafanikio waliyoyapata kama halmashauri lakini kumekuwepo na migogoro ya ardhi ya mara kwa mara ambayo wameweka mikakati ya kuitatua ikiwemo njia ya utoaji elimu.

Diwani wa Kata ya Njombe Mjini, Alatanga Nyagawa alisema anaamini kata yake imekuwa na mchango mkubwa katika pato la halmashauri kwani kwa sasa kuna ongezeko la wafanyabiashara wengi zaidi kutoka maeneo mbalimbali.

# Vyuo vikuu, kati vyatakiwa kuandaa mitaala ya Kiingereza

**Na Grace Mwakalinga,** KATAVI

VYUO vikuu na vya kati vya ualimu nchini vimeshauriwa kuandaa mitaala ya lugha ya Kiingereza kwa ajili ya kuwasaidia walimu wanaofundisha masomo ya sayansi na hisabati ili wafundishe kwa ufasaha zaidi.

Ushauri huo ulitolewa kutokana na tatizo linalojitokeza katika matumizi ya Lugha ya Kiingereza katika ufundishaji wa masomo hayo na kwamba walimu wengi hawakuandaliwa ipasavyo kutumia lugha hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana katika mafunzo endelevu ya walimu wanaofundisha sayansi na hisabati kutoka mikoa ya Songwe, Rukwa na Katavi, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Warwick kilichopo Uingereza, William Mwinuka, alisema kuwa vyuo vikuu vikianzisha mitaala maalumu ya lugha ya Kiingereza kwa walimu wa masomo haya, kutasaidia kuboresha ufundishaji, kuendana na mahitaji ya dunia na kuongeza ufaulu.

Mwinuka alieleza kuwa kwa sasa walimu wengi wanashindwa kumudu kutumia Kiingereza katika ufundishaji wa masomo ya sayansi na hisabati kwa sababu mfumo wa elimu vyuoni haukuwaandaa ipasavyo.

Alisisitiza umuhimu wa kuwa na mitaala maalum itakayowawezesha walimu hao kumudu kufundisha masomo yao kwa kutumia Kiingereza, ikijumuisha misamiati ya kisayansi ili kuboresha ufundishaji.

Aliongeza kuwa kwa mujibu wa utafiti alioufanya, Lugha ya Kiingereza inatumika kati ya asilimia 50 hadi 60 kufundishia kwa walimu wa masomo hayo, akisema kiwango cha kimataifa kinataka kiingereza kitumike asilimia 80 shuleni.

Alisema licha ya kiwango kidogo cha matumizi ya Kiingereza, mtaala wa sasa unaelekeza mitihani itungwe kwa lugha ya Kiingereza, jambo linalowaumiza wanafunzi, kwani hawajaandaliwa ipasavyo kutumia lugha hiyo.

Mwalimu wa somo la bailojia kutoka Shule ya Sekondari Myovizi iliyopo mkoani Songwe, Judith Oisso, alikubaliana na umuhimu wa Lugha ya Kiingereza katika ufundishaji wa masomo ya sayansi.

Alisema kuwa Lugha ya Kiingereza ni muhimu kwa wanafunzi kwani inawaandaa kwa kumudu ushindani wa soko la ajira ndani na nje ya nchi.

HABARI / KITAIFA

# Madai watoto kujiteka yaibua wataalamu

**Na Romana Mallya**

TUKIO la watoto wa miaka 16 na 12 kudaiwa kujiteka ili kujipatia fedha, limewaamsha wataalamu wa afya na kuwashauri wazazi kubeba jukumu la malezi.

Pia wameshauri kwamba yanapotokea matukio kama hayo wasiyapuuze bali watafute wasaikolojia tiba ili kumrejesha mtoto katika maadili.

Juzi, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Saalam lilitoa taarifa kuhusu watoto wawili kudaiwa kutoa taarifa za uongo za kutengeneza mazingira kuwa wametekwa na kwamba wanatakiwa kutoa fedha ili kwachiwe.

Watoto hao ni wanafunzi wa kidato cha pili na wa darasa la saba, wote wakazi wa Vijibweni, Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, Watoto hao walifanya hivyo ili kujipatia fedha kutoka kwa wazazi wao.

Daktari Bingwa Mbobezi wa Afya na Magonjwa ya Akili kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Saidi Kuganda, akizungumza na mwandishi wa habari hii jana kuhusu tukio hilo, alisema watoto wenye umri huo kufanya matukio ya aina hiyo ni kawaida.

Mtaalam huyo aliwaonya wazazi kuhakikisha matukio kama hayo yanapotokea wasiyafumbie macho bali wawatafute wasaikolojia tiba ili kuwasaidia watoto wasiendeleze vitendo hivyo hadi ukubwani na kujikita katika malezi bora.

"Hii ni tabia ya kawaida kwa watoto wenye umri kama wa hao watoto. Huwa na tabia za kujaribu kila kitu kwa kudhani wameshakua. Hawahofii kitu, hutengeneza stori (Habari) ambazo unaweza kudhani ni za kweli kumbe ni uongo mtupu.

"Ni vizuri mzazi anapoona hili kuchukua hatua haraka za kukutana na msaikolojia tiba ili kumsaidia mtoto kisaikolojia na kumrekebisha badala ya kumwacha katika ukuaji huo ambao baadaye unazalisha watu wasio na maadili mema," alishauri.

Kadhalika, aliwashauri wazazi na walezi kurejea katika sehemu yao ya malezi ya watoto wao kwa sababu baadhi hujifunza kutoka kwao.

Mtaalam huyo alisema mzazi au mlezi anapomwona mtoto ametumbukia katika matukio kama hayo wasijenge wasiwasi, bali waangalie njia bora na sahihi za kuwasaidia.

Mmoja wa wazazi, Yusuph Ali, mkazi wa Temeke, Dar es Salaam, alisema ukosefu wa maadili kwa watoto unachangia kundi hilo kujilea wenyewe na mwisho wa siku



kutumbukia katika mazingira hatarishi.

"Unajiuliza mzazi au mlezi hadi mtoto wako wa shule ya msingi au sekondari anafikia hatua ya kukaa chini na kupanga tukio kama hili, uko wapi? Una mchango gani katika malezi yake? Au maji yanafuata mkondo?," alisema.

Ali alisema ni muhimu wazazi kubeba jukumu kamili la malezi ili jamii ipate watoto bora wenye maadili ambao watakuja kuwa baba au mama wa baadaye.

"Tunapomuona kiongozi fulani anang'ara ametengenezwa kuanzia ngazi ya familia. Tusitegemee miujiza, yaani mtoto umwache ajilee hadi anafikia umri wa miaka 18 alafu utegemee awe mama au baba bora au mwalimu bora, daktari bora, mfanyakazi bora. "Miujiza hii utaishia kuiota, unazalisha mbegu mbaya ndani ya jamii ambayo haifutiki baadaye, tubebe jukumu la malezi bora," alisema.

Gerson Haule, mkazi wa Kinondoni, Dar es Salaam, aliwaomba wanawake na wanaume kubeba jukumu la malezi ya watoto hata kama wanakuwa kwenye shughuli za utafutaji.

"Unatafuta fedha sawa, lakini leo umekuwa tajiri huku watoto wako hawana maadili mema wengine wamegeuka dada poa, wengine wametumbukia kwenye dawa za kulevya na wengine wamegeuka wahalifu, kuna faida gani ya kile unachokitafuta kwa jasho," alihoji.

Alisema ni wajibu wa kila mzazi bila kujali jinsia kuhakikisha anabeba jukumu la malezi ya mtoto/watoto wao nyakati zote.

Kadhalika, aliikumbusha jamii ule usemi kuwa, 'mtoto wa mwezio muone kama mtoto wako' inapaswa kuzingatiwa ili anapoona mtoto wa jirani anakwenda nje ya maadili ya Mtanzania abebe jukumu la kumwonya kama vile angefanya kwa mwanaye.

Fransisca Peter, mkazi wa Tegeta, wilayani Kinondoni, alikumbusha kuwa huko nyuma majukumu ya malezi kwa kiwango kikubwa yalifanywa na mama kwa sababu alibaki nyumbani na baba alikuwa mtafutaji.

Alisema kwa sasa kutokana na wazazi wote wawili kuingia kwenye utafutaji, muda mwingi watoto hujilea wenyewe.

"Lakini hiki hakiwezi kuwa kisingizio kwetu wazazi, tunawajibu wa asilimia 100 wa kuhakikisha watoto tunaowalea hadi kuondoka katika mikono yetu na Kwenda kujitegemea wanakuwa mikono salama.

"Ndiyo maana kuna usemi, 'Mtoto kwa mama hakui' unamuonya hata kama ana ndevu zake, amekosea unamrudisha kwenye mstari ili awe baba au mama bora au kiongozi mwenye maadili yote," alisema.

Alitoa wito kwa wazazi kutenga muda wa kutosha wa kukaa na watoto na kuwafundisha maadili mema na kutumia nyumba za ibada ipasavyo ili wajifunze neno la Mungu litakalowajengea hofu ya kutenda mabaya.

Katika taarifa ya Jeshi la Polisi, Kamanda Muliro alisema baada ya taarifa hiyo katika mahojiano ya kina watoto hao walidai walifanya hivyo ili kupata fedha kutoka kwa wazazi wao.

"Walitoweka Januari 26, mwaka huu, kuelekea Longoni Beach na walikesha huko hadi siku iliyofuata na baadaye walielekea Tungi hadi walipowapata wakizunguka Januari 29, mwaka huu ," anasema.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda anasema Jeshi la Polisi linalaani vitendo hivyo vya watu wenye lengo la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji

ISO 9001:2015 Certified

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu Na. 126 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni Na. 5(1) ya Kanuni za Mafuta (Compressed Natural Gas) (Supply and Marketing Services Rules, GN No. 220 of 2019).**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi la kibali cha ujenzi wa kituo cha kujaza gesi asilia iliyoshindiliwa kwenye magari kutoka **TAN HEALTH TANZANIA LIMITED** kitakacho jengwa kiwanja namba 583 eneo la Mbezi Beach, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam.

Hivyo, Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

218365802

EWURA House, 3 EWURA Street, 41104 Tambukareli, P.O. Box 2857, Dodoma, Tanzania
Tel: +255 26 2329002 – 4 • Fax: +255 26 2329005 • E-mail: info@ewura.go tz



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji

ISO 9001:2015 Certified

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu Na. 126 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni Na. 5(1) ya Kanuni za Mafuta (Compressed Natural Gas) (Supply and Marketing Services Rules, GN No. 220 of 2019).**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi kutoka kwa **KING LION INVESTMENT COMPANY LIMITED** ya kibali cha ujenzi wa kituo kidogo cha kupokea gesi asilia iliyoshindiliwa kitakacho jengwa kiwanja namba 552 eneo la kiwanda cha **KING LION INVESTMENT Co. Ltd** kilichopo Zegereni, Wilaya ya Kibaha, mkoani Pwani. Gesi asilia hii itatumika kama nishati kiwandani kwa ajili ya kuendeshea boiler.

Hivyo, Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

218365802

EWURA House, 3 EWURA Street, 41104 Tambukareli, P.O. Box 2857, Dodoma, Tanzania
Tel: +255 26 2329002 – 4 • Fax: +255 26 2329005 • E-mail: info@ewura.go tz

# Nyama ya nguruwe isiyoiva yatajwa kusababisha shida ugonjwa kifafa

**Na Christina Mwakangale**

ULAJI wa nyama ya nguruwe isiyoiva ipasavyo, ajali, uzazi pingamizi na mbung'o vimetajwa kuwa vyanzo vya kuenea kwa ugonjwa wa kifafa.

Pia imebainika kuwa wagonjwa wengi wanaosumbuliwa na ugonjwa huo wako Ulanga, mkoani Morogoro na Hydom, Manyara.

Kutokana na hali hiyo, Chama cha Wataalamu wa Kifafa Tanzania (TEA), kimechukua hatua kadhaa ikiwamo kuanzisha mradi wa kituo cha mafunzo ya tiba saidizi na ujuzi huko Mahenge wilayani Ulanga.

Bingwa wa Ubongo, Uti wa Mgongo na Mishipa ya Fahamu, Dk. Patience Njenje, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam, alipozungumza na vyombo vya habari kuhusu Siku ya Kifafa Duniani, itayaoadhimishwa Februari 10, mwaka huu.

"Duniani kote kifafa ni ugonjwa wa kudumu wa ubongo unaoathiri takribani watu milioni 60, huku ukiathiri watu 34-76 kwa kila wagonjwa 100,000 wapya wanaoongezeka kila mwaka, ukiwa na wastani wa uwiano wa asilimia 0.5 hadi moja.

"Nchini Tanzania athari ya jumla ya muda wote ni asilimia mbili. Afrika ina idadi kubwa ya walioathirika ikiwa ni kati ya watu 20 hadi 58 kwa kila watu 1000. Utafiti uliopita na wa sasa umegundua kuwa takribani watu milioni moja wanaishi na kifafa nchini. Mahenge huko Ulanga na Hydom wilayani Mbulu kuna wagonjwa wengi zaidi," alisema.

Alisema maeneo ambayo yana idadi kubwa ya wagonjwa, sababu mojawapo ni za kijiografia zikiwamo kuwapo maambukizi kutokana na nzi aina ya mbung'o Pamoja na Hydom ambako kuna ulaji zaidi wa nyama ya nguruwe.

"Tanzania ni moja ya nchi zenye baadhi ya vijiji vyenye idadi kubwa ya walioathirika hadi kufikia watu 37.5 kwa kila watu 1000, ikiwa na watu 73 hadi 111 kwa kila wagonjwa 100,000 wapya wanaoongezeka kila mwaka.

"Kitimoto (nyama ya nguruwe) isipoiva ipasavyo, husababiosha minyoo ambayo husafiri hadi kichwani na kuziba damu kupita ipasavyo. Uzazi pingamizi, yaani mjamzito anapata tabu sana wakati wa kujifungua. Ajali ni sababu nyingine na wagonjwa wengi ni vijana, pengine mtoto alidondoka akiwa mdogo na kapata uvimbe baadaye anaanza kupoteza fahamu," alisema.

Dk. Njenje, alisema yako mafanikio baada ya matokeo ya sasa ya utafiti kuonesha kupungua kwa idadi ya waathirika kutoka zaidi ya 70 hadi 20 au 15 kwa kila watu 1,000 na waathirika wapya kutoka zaidi ya 70 hadi karibia 50 kwa kila watu 100,000 kwa mwaka katika baadhi ya maeneo nchini.

"Kwa sasa kiwango cha vifo kwa wagonjwa kimeshuka kutoka kiwango kikubwa cha mara sita zaidi hadi mara nne, ikilinganishwa na kiwango cha vifo kwa watu wote. Wenye kifafa ni watu wenye umri mndogo wakiwa na wastani wa umri wa miaka 15.4 hali ambayo imebakia sawia na matokeo ya miaka 60 na 32 iliyopita," alisema.

Dk. Njenje alisema asilimia 60 ya watu wenye kifafa huenda kituo rasmi cha kutolea huduma za afya kwa wastani wa mwaka mmoja kutoka degedege la kwanza.

Ni asilimia tano hadi 10 tu ndio hupata dawa sahihi na za mara kwa mara, hivyo pengo la ugunduzi na matibabu likibakia kubwa na mwenendo unaopungua katika maeneo baadhi kutoka asilimia 100 miaka 60 iliyopita hadi 95 miaka 30 iliyopita na kwa sasa ni takribani asilimia 50.

"Watu wenye kifafa walio kwenye umri wa kuoa au kuolewa, asilimia 67 hawajaoa au kuolewa. Kati ya asilimia 33 waliooa au kuolewa wana viwango vikubwa zaidi vya talaka. Karibu asilimia 24 ya watu wanaoishi na kifafa ni walemavu, kutokana na sababu zinazotokana na au kama matokeo ya dalili za kifafa (kukakamaa maungio kutokana na kuungua, makovu, majeraha ya kichwa," alisema.

"Kwa sasa hatuna vituo rasmi vya tiba saidizi kwa watu wanaoishi na Kifafa isipokuwa vituo vitatu, vinavyoendeshwa na shirika lisilo la kiserikali katika vituo vya Kanisa Katoliki.

# Kesi Kocha wa Makipa Simba yanguruma Korti ya Mafisadi

**Na Kulwa Mzee**

KESI ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroine kilo 34.89 inayomkabili aliyekuwa Kocha wa Makipa wa Klabu ya Simba, Muharami Sultani na wenzake watano, imeanza kunguruma Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu, washtakiwa wakikana mashtaka.

Mmiliki wa Kituo cha Michezo cha Cambianso kilichoko Tuangoma, Kigamboni mkoani Dar es Salaam, Kambi Zubery amekana kuongoza wenzake kufanya biashara ya dawa za kulevya na amekana kukamatwa mpakani Horohoro, Tanga akitaka kutorokea Kenya.

Hayo yalibainishwa jana mbele ya Jaji Godfrey Isaya wakati washtakiwa wakisomewa mashtaka na maelezo ya awali ya kesi inayowakabili.

Akisoma mashtaka, Wakili wa Serikali Tully Helela alidai washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka manane; kati ya mwaka 2016 na Novemba 2022, maeneo ya Dar es Salaam na Mkuranga, wote wanadaiwa kuongoza genge la uhalifu na kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroine.

Mshtakiwa Kambi anakabiliwa na mashtaka matano kati ya manane ya kutakatisha fedha, ikidaiwa alijipatia magari matano aina ya Tata wakati akijua mali hizo zimetokana na mazalia ya kosa la kuongoza genge la uhalifu.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Kambi, Sultani, Maulid Mzungu, maarufu Mbonde, Said Matwiko, John Andrew maarufu Chipanda ambaye ni mfanyakazi wa Cambiasso na Sara Joseph ambaye ni mke wa Matwiko.

Akisoma maelezo ya awali, Wakili Tully alidai maofisa wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kuzuia Dawa za Kulevya (DCEA), wakiwa kwenye doria maeneo ya Kivule, walipata taarifa ya watu wanasafirisha dawa za kulevya.

Alidai mtoa taarifa aliwaongoza nyumbani kwa mshtakiwa Matwiko na kundi lingine lilielekea Kitunda Magole kwa mshtakiwa John.

Ilidaiwa katika kufanya upekuzi nyumbani kwa Saidi, walikuta pakiti 27 zilizodhaniwa kuwa dawa za kulevya, mshtakiwa Saidi na Sarah walikamatwa na vielelezo vilipelekwa kwa Mkemia kwa ajili ya uchunguzi ambako ilibainika ni dawa za kulevya aina ya heroine.

Ilidaiwa pia upekuzi ulifanyika nyumbani kwa washtakiwa wengine wote na nyumbani kwa Maulid kulikutwa pakiti nane za dawa za kulevya.

Mshtakiwa Kambi alidai kuwa wakati wa upekuzi unafanyika nyumbani kwake, hakuwapo na zilichukuliwa Sh. milioni tisa na gari na kwamba si kweli kwamba simu nne zilikutwa nyumbani kwake.

Alidai hakukamatwa katika Mpaka wa Horohoro, Tanga akitaka kukimbilia Kenya bali alikamatwa maeneo karibu na Horohoro.

Mshtakiwa Kambi alikana kuwafahamu washtakiwa wengine wote lakini mshtakiwa wa pili na watatu walikubali kwamba wao ni ndugu na mshtakiwa wa nne alikubali kwamba mshtakiwa wa sita ni mke wake.

**FRONTANA ENTERPRISES LIMITED.**
**Certificate of Incorporation Regulation Number: 172481256**

At the **Ordinary meeting** of Members (Shareholder's) of **FRONTANA ENTERPRISES LIMITED** hold at the registered office of the company on 31 January 2025 the following resolutions was duly passed.

**PRESENT:**
- FRONTO BENEDICT FURAHA Chairman/Shareholder
- ANASTASIA JUSTIN OLOMI Company Secretary/Shareholder

**BOARD RESOLUTION OF WINDING-UP THE COMPANY**

It was **RESOLVED** by the Board of the company that;
1. The Board decides to wind-up the Company due to the economic situation, thus unable to start operations.

**IT IS HEREBY CERTIFIED** that the above resolutions were dully passed in accordance with and in compliance with the memorandum and articles of the company.

Dated at Dar Es Salaam this 31 Day of January 2025

FRONTO BENEDICT FURAHA
Chairman

ANASTASIA JUSTIN OLOMI
Secretary

**FRONTANA FINANCE LIMITED.**
**Certificate of Incorporation Regulation Number: 172473229**

At the **Ordinary meeting** of Members (Shareholder's) of **FRONTANA FINANCE LIMITED** hold at the registered office of the company on 31 January 2025 the following resolutions was duly passed.

**PRESENT:**
- FRONTO BENEDICT FURAHA Chairman/Shareholder
- ANASTASIA JUSTIN OLOMI Company Secretary/Shareholder

**BOARD RESOLUTION OF WINDING-UP THE COMPANY**

It was **RESOLVED** by the Board of the company that;
1. The Board decides to wind-up the Company due to the economic situation, thus unable to start operations.

**IT IS HEREBY CERTIFIED** that the above resolutions were dully passed in accordance with and in compliance with the memorandum and articles of the company.

Dated at Dar Es Salaam this 31 Day of January 2025

FRONTO BENEDICT FURAHA
Chairman

ANASTASIA JUSTIN OLOMI
Secretary

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHARI DODOMA**
**MAOMBI MADOGO NA. 276 YA MWAKA 2024**
**DR. GASPER MWEMBEZI....................................MDAI**
**DHIDI YA**
**1. MARIA WILSON PETER............**
**2. LUSAKO KILEMBE.....................** } **WADAIWA**

**KWA:**
**MARIA WILSON PETER**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hil.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 06.02.2025 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:-** Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo 04 ya Mwezi February, 2025.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**YAH: MADAI NO. 404/2024**

**MDAI: 21 CENTURY FF (LUDOVICK TIMOTH)**

**MDAIWA: JAFFARI IBRAHIM CHIVALO**

**Ndugu JAFFARI IBRAHIM CHIVALO –** Popote pale ulipo unaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria mnamo tarehe 11/02/2025 bila kukosa.

Kama hutohudhuria basi shauri hili litasikilizwa upande mmoja na uamuzi kutolewa.

PRIMARY COURT TEMEKE DAR ES SALAAM
HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO TEMEKE
MAHAKAMA YA MWANZO TEMEKE

**KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA**



**NEEMA HAMISI JUMA** naomba kutangaza kupotelewa kwa hati yangu ya kusafiria namba **TAE565204** iliyotolewa uhamiaji makao makuu Mnamo tarehe 09/03/2023. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taaria ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/21691/2025.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**YAH: SHAURI LA MADAI NA. 79/2019**

**MDAI............PUNUNTA'S COMPANY LTD**

**DHIDI YA**

**MDAIWA..............MUSSA MBUYA**

Unaamriwa na Mahakama ya Mwanzo Mjini Mwanza kufika tarehe 24/02/2025 saa 2:30 asubuhi bila kukosa ili kujibu madai yaliyofunguliwa hapa Mahakamani, endapo hutafika Mahakama shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.

HAKIMU MWANDAMIZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MWANZA

**KUPOTEA KWA VYETI**



**RAINA LONGINO KAJUMBURA** anatangaza kupotelewa na Certificate of Enrollment chenye PIN number **0404424.** Certificate of Diploma chenye namba **S1689/0061/2014** vilivyotolewa na **KAMPALA INTERNATIONAL UNIVERSITY** mwaka 2020. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/197653/2025.**

**KUPOTEA KWA PASSPORT**



**SAULO MICHAEL FIDELY** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye namba tae **615835** iliyotolewa tarehe 04.08.2023. Kwa yeyote ambaye atakayeiona atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/MWA/ILE/50407/2024.**



Raia wa DRC wakiwa na hofu wakiwasili katika kambi ya wakimbizi ya Gisenyi, wakikimbia mapigano mashariki ya Congo. **PICH: AFP**

# Matumaini mapya yatarajiwa mkutano SADC, EAC Dar

**Na Moshi Lusonzo**

WAKATI viongozi wa kikanda wa Jumuiya za Afrika Mashariki (EAC) na Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) watakutana, kujadili hatima ya mgogoro wa waasi wa M23 Congo, wachambuzi wasisitiza cha muhimu ni kufahamu mzizi wa tatizo.

Marais Paul Kagame wa Rwanda na Felix Tshisekedi wa DRC, ambao wanatuhumiana kuhusu mapigano ni wajumbe mahususi wa mkutano huo utakaofanyika Jumamosi, jijini Dar es Salaam.

Baadhi ya wachambuzi wa masuala ya kisiasa za kikanda, waliochambua mkutano utakaohudhuriwa na marais wa nchi zote za jumuiya hizo, walisema viongozi hao wachukue hatua madhubuti ya kuchimbua mzizi wa tatizo na kutoa uamuzi utakaorudisha utulivu katika eneo la kikanda.

Wakizungumza na Nipashe Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, George Kahangwa, alisema mgogoro huo wa mashariki mwa DRC, umedumu kwa muda mrefu, umefika wakati viongozi kusema basi wakati watakapokutana.

Alisema jambo jema ni viongozi hao wa Rwanda na DRC kukubali kuhudhuria, hivyo kila upande utatoa hoja za ana kwa ana zitakazosaidia kujua kiini cha pande hizo mbili kugombana.

Kahangwa alisema anatazamia kuona matokeo chanya yanapatikana kusaidia kumaliza mapigano hayo yanayotishia kutoweka kwa utulivu wa kikanda.

"Mgogoro huo ni wa muda mrefu, ulianza katika kipindi cha ukoloni hadi wakati mataifa ya Rwanda na DRC yalipopata uhuru. Jambo la muhimu hapa kutumia nafasi hii kupata ufumbuzi wa kweli ambao utasaidia kutuliza eneo la mashariki mwa DRC ambalo lina utajiri wa madini," amesema Kahangwa.

Kahangwa alisema mgogoro huo ambao umefikia hatua mbaya usipopatiwa ufumbuzi wa haraka, unaweza kuleta athari za kiuchumi na kijamii kwa mataifa ya jirani ikiwamo Tanzania.

> Uganda wiki iliyopita ilipeleka zaidi ya wanajeshi 1,000 wa ziada mashariki mwa DRC, karibu na eneo ambalo kuna mapigano kati ya jeshi la serikali na waasi wa M23.

Alisema kwa kutumia mkutano huo kila pande zinazolaumiana, ziwasilishe ushahidi wa kutosha kuthibitisha madai hayo ili kurahisisha viongozi hao kutoa maamuzi yasiyoegemea upande wowote na utakaomaliza mgogoro huo.

"Mkutano usiwe wa kuonyeshana vidole, kila upande uulizwe na kutoa ushahidi wa kutosha kuhusu madai yao ili uamuzi utakaotolewa ulete tija na suluhu ya kudumu," aliongeza Kahagwa.

Abdulkarim Atiki, alisema kutokana na kasi ya waasi wa M23 kuchukua maeneo Kivu Kaskazini, mazungumzo pekee yatasaidia kupatikana kwa amani na sio kutumia nguvu za kijeshi.

"Viongozi wetu watambue kuwa M23 wana nguvu kubwa kijeshi, kupambana nao kwa silaha sio jambo jepesi kutokana na waasi wanatumia silaha za kisasa, alisema Atiki.

Alisema mgogoro huo licha ya kuathiri mataifa jirani na DRC, kuna baadhi ya mataifa na kampuni za nje zinanufaika kwa kutorosha madini yenye thamani.

**HOFU YATANDA**

Wakati huo huo, imeelezwa hofu imeongezeka kuhusu uwezekano wa waasi wa M23 kusonga mbele na kuuteka mji wa Bukavu, ambao uko Kivu Kusini.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Ujerumani (DW), Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa linajiandaa kufanya kikao cha dharura kesho, kuujadili mgogoro wa mashariki mwa Congo.

Msemaji wa baraza, Paschal Sim aliwaambia waandishi wa habari mjini Geneva kwamba kikao hicho kimeitishwa kufuatia ombi la serikali ya DRC lililotolewa Jumatatu.

Baraza hilo kimsingi ndio chombo cha juu zaidi katika Umoja wa Mataifa kinachohusika na masuala ya haki za binadamu.

Ingawa waasi wa M23 kutangaza kusimamisha mapigano, bado machafuko yalienea katika mkoa jirani wa Kivu Kusini na kusababisha raia kuwa na hofu kwamba kundi hilo la waasi linasonga mbele kuelekea mji wa Bukavu.

Fazili Mubole, ofisa wa shirika moja la kiraia alisema taarifa iliyotolewa na M23 kuwa wanasimamisha mapigano wanaona kama mkakati wao wa kijeshi.

"Wanaposema kwamba mji wa Bukavu hawawezi kuuchukua, huo ni mkakati wao wa kujiimarisha, na kujipanga upya kwa wapiganaji na silaha na hapo hapo wakisonga mbele kuelekea kuuchukuwa mji wa Bukavu. Na ndio sababu bado tunaziomba mamlaka kutoiamini taarifa kama hii na inatakiwa mamlaka iwe tayari kuwamaliza maadui wa jamhuri." Alisema.

Jumatatu waasi wa M23 walitangaza kusitisha mapigano kwa lengo la kupisha shughuli za kibinadamu. Tangazo hilo lilitolewa siku kadhaa kabla ya kufanyika mkutano utakaowakutanisha Rais Felix Tshisekedi na Paul Kagame.

**UGANDA YATUMA KIKOSI**

Uganda wiki iliyopita ilipeleka zaidi ya wanajeshi 1,000 wa ziada mashariki mwa DRC, karibu na eneo ambalo kuna mapigano kati ya jeshi la serikali na waasi wa M23.

Hayo ni kwa mujibu wa vyanzo vinne vya kidiplomasia vya Umoja wa Mataifa. Hatua hiyo imezidisha wasiwasi kupanuka kwa mgogoro huo na kuwa wa kanda nzima.

Aidha, mamia ya Wakongo walijitokeza jana kuandamana mbele ya ofisi za Umoja wa Ulaya nchini Afrika Kusini kudai Rwanda iwekewe vikwazo, kutokana na hatua yake ya kuwaunga mkono waasi wa M23.

Takriban waandamanaji 2,000 wakiwa na mavazi ya rangi za bendera ya nchi yao Congo, buluu, njano na nyekundu walisikika wakiimba nje ya ubalozi wa Umoja wa Ulaya ulioko katika mji mkuu wa Pretoria.

Waandamanaji hao walishikilia mabango yaliyoandikwa ujumbe wa kutaka nchi yao iwe huru na kuutambua mchango wa kikosi cha jeshi la Afrika Kusini wanaojaribu kulikomboa eneo la mashariki.

Waandamanaji walisikika wakiutaka Umoja wa Ulaya kuweka vikwazo dhidi ya Rwanda kama walivyofanya dhidi ya Russia kufuatia vita vinavyoendelea Ukraine.

# SIMBA QUEENS, JKT NA VITA YA UBINGWA TWPL

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI 'Maafande' wa JKT Queens wakitoa dozi kali kwa kuichapa Mlandizi Queens mabao 12-0, vita yao ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake msimu huu dhidi ya mabingwa watetezi, Simba Queens, imeendelea kuimarika.

JKT Queens yenye mchezo mmoja mkononi imefikisha pointi 29 wakati Simba Queens ambayo ilipata bao la 'jioni' kupitia mshambuliaji wake tegemeo, Jentrix Shikangwa, iliwafungwa Ceasiaa goli 1-0 katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Simba Queens imeendelea kukaa kileleni katika msimamo wa ligi hiyo ikifikisha pointi 34, imeshinda michezo 11 na imetoka sare mara moja msimu huu.

**Nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo yenye timu 10 inashikiliwa na JKT Queens huku Yanga Princess ambayo ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mashujaa Queens iko katika nafasi ya tatu baada ya kufikisha pointi 21 hapo juzi.**

Bunda Queens kutoka mkoani Mara yenye pointi tisa sawa na Gets Program ya jijini, Dodoma na Mlandizi Queens yenye pointi moja zinaburuza mkia katika ligi hiyo ya juu kwa wanawake hapa Tanzania Bara.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Yusif Basigi, aliliambia gazeti hili mechi hiyo ilikuwa ngumu lakini wachezaji wake walipambana katika muda wote wa mchezo.

Basigi alisema wamejiandaa kukutana na ushindani katika kila mechi wanayocheza na hiyo inawasaidia kujiimarisha katika kusaka ushindi.

"Ilikuwa mechi ngumu sana, wapinzani wetu wana kikosi kizuri, waliingia na mipango yao ya kutuzuia, lakini sisi pia tulikuwa tunatafuta njia ya kuwatoka, tutaendelea kujiimarisha ili kuhakikisha tunafikia malengo yetu, tunajua ili kuwa bingwa ni lazima tushinde mechi zote," Basigi alisema.

Naye Shikangwa alisema amefurahi timu yao kupata ushindi katika mechi hiyo na hii imetokana na wachezaji kujituma na kutokata tamaa.

"Huwa tunasema tunatakiwa kupambana mpaka mechi itakapomalizika, tunajua kila mechi kwetu ni sawa na fainali, tulipambana na tutaendelea kupambana katika mechi zote zilizobakia," Shikangwa alisema.

Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itasimama kwa muda wa wiki tatu ili kupisha maandalizi ya Timu ya Taifa (Twiga Stars), ambayo inajiandaa kuikaribisha Equatorial Guinea katika mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (WAFCON), itakayochezwa Februari 20, mwaka huu hapa jijini.

# Stand Utd yazidi kutakata

**Na Adam Fungamwango**

VITA ya kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara inaendelea katika Ligi ya Championship, baada ya Stand United kuichapa Transit Camp mabao 3-0, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani juzi.

Mabao ya washindi yalifungwa na Kigi Makasi, Selemani Rashid na Omari Bebartov.

Ushindi huo umeifanya ligi hiyo iwe ngumu na usiyotabirika, baada ya Stand United kufikisha pointi 35, ambazo ni sawa na ilizokuwa nazo Mbeya City, Geita Gold, yenye pointi 36 iko kwenye nafasi ya pili huku Mtibwa Sugar ikiongoza na pointi zake 44.

Ukiondoa, TMA, timu zote zilizobaki, kuanzia ya kwanza hadi ya sita, zimeshawahi kucheza Ligi Kuu kwa nyakati tofauti kabla ya kushuka daraja, huku Mtibwa na Geita Gold zikiwa zimeteremka msimu uliopita.

Hatari ya kushuka daraja inainyemelea Biashara United, ambayo mpaka sasa ina pointi nne baada ya kushuka dimbani katika michezo 17.

Biashara United, iliyoshuka daraja kutoka Ligi Kuu Bara msimu wa 2021/2022, ilipokonywa pointi 15 na Bodi ya Ligi baada ya kushindwa kufika katika mchezo wa ligi hiyo dhidi ya Mbeya City uliotarajiwa kufanyika Desemba Mosi, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya.



Kiungo wa Yanga Princess, Agness Palangyo (kushoto), akimpiga chenga beki wa kati wa Mashujaa Queens, Zabela katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Isamuhyo, Dar es Salaam juzi. Yanga Princess ilipata ushindi wa mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# KVZ FC hesabu kali ubingwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KATIKA kuhakikisha inafikia malengo yake ya kutwaa ubingwa, uongozi wa KVZ FC umesema wanaichukulia kwa 'uzito mkubwa' michezo yote Ligi Kuu Zanzibar inayoendelea katika viwanja mbalimbali visiwani hapa, imeelezwa.

KVZ itaikaribisha Mwenge katika mechi ya raundi ya 17 ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Kiwengwa.

KVZ FC yenye pointi 29 ni moja ya timu zilizo katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu ikiwa kwenye nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo sawa na Muembe Makumbi City ambao iliyoko juu yao kutokana na uwiano mzuri wa mabao.

Vinara wa ligi hiyo yenye timu 16 ni Mlandege FC yenye pointi 31.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa KVZ, Abduljalili Mohamed, alisema katika mzunguko wa pili timu haitakiwi 'kuzubaa' au kuzingatia ushindi wanapocheza nyumbani na badala yake wanatakiwa kupambana ili kushinda kila mchezo.

Mohamed alisema mzunguko wa lala salama ni mgumu kutokana na upinzani ulioko kwa timu unayokutana nayo bila kujali iko katika nafasi gani kwenye msimamo wa ligi.

Alisema wachezaji na benchi la ufundi wanajua wanachotakiwa kukifanya ili kufikia malengo ya klabu na mashabiki wao na ndio maana wanaonyesha ushindani wa namba kuanzia wanapokuwa mazoezini.

"Tunahitaji kufikia malengo yetu ya kutwaa ubingwa, tumajua ugumu na ushindani uliopo, tunafahamu lala salama kila mechi ni ngumu, lakini wachezaji wetu wanajua tunachohitaji katika msimu huu ndio maana timu imekuwa na hari kubwa uwanjani," alisema ofisa huyo.

Aliongeza kila mchezo ambao wanashuka uwanjani kwao wao wanauchukulia kama fainali ili kwa ajili ya kuhakikisha wanapata pointi tatu.

"Hakuna mchezo ambao tutaudharau katika mzunguko huu, mpango wetu ni kupata alama tatu, ndio maana hatuangalii ukubwa au udogo wa timu, mifumo yetu ni kupata ushindi tu," ofisa huyo alisema.

Bingwa wa Ligi Kuu Zanzibar hupata nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GERNACHO, MAINOO SOKONI

MANCHESTER United bado iko tayari kumuuza winga wa Argentina, Alejandro Garnacho mwenye umri wa miaka 20, na kiungo wa kati wa England, Kobbie Mainoo (19) msimu wa kiangazi. ***(Guardian)***

### CUNHA NJIA MOJA

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Matheus Cunha, 25, ameonyesha nia ya kuhamia klabu kubwa licha ya kusaini mkataba mpya wa Wolves. ***(Football Insider)***

### FOREST YAIGOMEA CHELSEA

NOTTINGHAM Forest ilikataa ofa ya siku ya mwisho kutoka kwa Chelsea kwa mlinzi wa Brazil, Murillo, 22. Ingekuwa mauzo ya rekodi ya klabu. ***(Telegraph)***

### AWAKATAA WATURUKI

MSHAMBULIAJI wa Manchester United na England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 27, alikataa kuhamia klabu moja ya Uturuki kabla ya kujiunga na Aston Villa kwa mkopo. ***(Manchester Evening News)***

### NIKE KUMTOSA RASHFORD

MARCUS Rashford anaweza kupoteza asilimia 100 ya fedha za udhamini anazopokea kutoka kwa Nike kwa sababu kampuni hiyo kubwa ya mavazi ya michezo inaichukulia Aston Villa kama klabu ndogo ikilinganishwa na Manchester United. ***(Mail Plus)***

### OLD TRAFFORD KUNOGESHWA

WACHAMBUZI wanaamini inaweza kufika hadi mwaka 2032 kabla ya Uwanja wa Old Trafford unaomilikiwa na Manchester United kujengwa kikamilifu au kuendelezwa upya. ***(Mail Plus)***

### BARCA, PORTO WAMALIZANA

BARCELONA haikupokea pauni milioni 8.5 kutokana na mauzo ya kiungo wa kati wa Porto, Nico Gonzalez, 23, kwenda Manchester City, kwa sababu klabu hiyo ililipa klabu hiyo ya Katalunya ada ya pauni milioni 2.5 ili kupunguza nusu ya kipengele cha mauzo. ***(ESPN)***

### NEWCASTLE KUJENGA UWANJA

KLABU ya Newcastle United inategemea kujenga uwanja mpya karibu na St James' Park. ***(Telegraph)***

### UNITED YAIBANIA BENFICA

MANCHESTER United inataka kukataa ofa ya mkopo ya Benfica kwa ajili ya mlinzi wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Tyrell Malacia, 25. ***(Mail Plus)***

### ARTETA AMTAKA WILLIAMS

WINGA wa Athletic Bilbao na Timu ya Taifa ya Hispania, Nico Williams, 22, ni kipaumbele cha usajili wa kocha wa Arsenal, Mikel Arteta. ***(Football transfer)***

### TRUFFETS KUTUA EPL

KLABU ya Everton inashughulikia mpango wa kumsajili beki wa kushoto wa Rennes na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Adrien Truffert, 23. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA: HAVERTZ KUIBEBA ARSENAL

**Kocha huyo asema wanatarajia kupata 'makubwa' ku...**

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amemtaja, Kai Havertz, ana 'vinasaba' vya nguvu ya kupambana na amemtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani kufidia baada ya kushindwa kwa Arsenal kusajili fowadi katika dirisha la Januari.

**Washikabunduki hao hawakuficha nia yao ya kutaka kuongeza mshambuliaji kutokana na majeruhi ya Bukayo Saka na Gabriel Jesus lakini hawakufanikiwa baada ya ofa ya pauni milioni 40 kukataliwa na Aston Villa kwa Ollie Watkins.**

Jesus anatazamiwa kuwa nje ya uwanja kwa muda wote uliosalia wa msimu huu baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti, huku Saka hatarajiwi kurejea hadi mwezi ujao, jambo ambalo linaweka mkazo zaidi kwa Havertz kuchukua jukumu muhimu wakati Arsenal ikipambana na majeruhi.

Kabla ya mechi ya nusu fainali ya Kombe la Carabao dhidi ya Newcastle United hapo jana, Arteta alimtaka Havertz kuchukua jukumu la kuibeba timu, akiwa amesajiliwa kwa pauni milioni 65 kutoka Chelsea mnamo mwaka, 2023.

"Ana uwezekano wa kuanza kila mchezo," alisema Arteta.

"Labda tunapitia hali hiyo na akafunga mabao mengine 15 au 18? Unaweza kufikiria? Hiyo ni hali nzuri.

"Ana vinasaba vya mtu mwenye nguvu. Ameundwa vizuri sana. Ni mchezaji ambaye chochote unachomwambia anafurahi kufanya, kukimbia katika eneo la sita.

"Anajua kipi kinamfaa na kisichofaa. Tunajua jinsi ya kumsimamia na tunaamini kuwa anaposema jambo ni kwa sababu sahihi, sio kwa sababu anataka kukwepa jambo."

Havertz amefunga mabao 15 na kusajili asisti tano katika mechi 33 msimu huu, lakini amekabiliwa na ukosoaji wa makosa kadhaa, haswa wakati Arsenal ikifungwa katika mechi tano mwezi uliopita.

# DAVIES AITOSA MADRID ASAINI BAYERN MUNICH



**MADRID,** Hispania

ALPHONSO Davies amekubali kusaini mkataba mpya na Bayern Munich, klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ilitangaza rasmi juzi na hivyo kumaliza harakati za Real Madrid za kumnasa mchezaji huyo kwa muda mrefu.

Mkataba wa sasa Davies na wababe hao wa Bavaria unamalizika mwisho wa msimu wa mwaka 2029/2030 na ungefanya kusalia kwake huko kufikie miaka 11.

"Nina furaha sana kwa kuongeza mkataba wangu katika klabu hii kubwa," alisema Davies katika taarifa ya habari.

"Nilikuja FC Bayern nikiwa na umri wa miaka 18 na nilitaka tu kujifunza mengi iwezekanavyo kila siku ili kuwa mmoja bora katika nafasi yangu. Sasa natazamia miaka mingine mitano pamoja. Tayari nimepata mafanikio mengi hapa, lakini kuna mengi zaidi yajayo."

ESPN iliripoti msimu uliopita wa joto Madrid ilitaka kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Canada mwenye umri wa miaka 24, ambaye mkataba wake wa awali ulipaswa kumalizika Juni, mwaka huu ikiwa makubaliano ya ada yanaweza kufikiwa na Bayern.

Wakati uhamisho huo haukutimia, Madrid walitaka kumnunua Davies kwa uhamisho wa bila malipo msimu huu wa joto kama sehemu ya marekebisho ya safu ya ulinzi ambayo wanatumaini pia kuwasili kwa Trent Alexander-Arnold, ambaye mkataba wake wa Liverpool pia unamalizika mwishoni mwa msimu.

"Alphonso Davies amekuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani katika nafasi yake hapa Bayern na amevutia watu wengi," alisema Mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo ya Ujerumani, Christoph Freund.

"Ukweli anataka kuendelea hapa kwetu unaonyesha hadhi ya Bayern katika soka la kimataifa na Alphonso amepata nyumba yake ya michezo mjini Munich."

Davies alikuwa bado anazingatia chaguzi zake mwezi uliopita, chanzo kiliiambia ESPN, kabla ya kuamua kubaki na upande wa Ujerumani.

# João Félix atua rasmi AC Milan




**MILAN,** Italia

AC Milan ilitangaza kukamilisha usajili wa João Félix kwa mkopo kutoka Chelsea kwa muda uliobakia kwa msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno aliwasili Milan juzi na kufaulu vipimo vya afya kabla ya kusaini mkataba na Rossoneri hao.

Félix mwenye umri wa miaka 25, alivutiwa na klabu nyingine kadhaa ikiwa ni pamoja na Aston Villa, lakini upendeleo wa Chelsea daima umekuwa kwa fowadi huyo kujiunga na klabu nje ya Uingereza.

Alijiunga na Chelsea Agosti iliyopita kwa mkataba wa Euro milioni 50 kutoka Atlético Madrid ili kuanza kipindi chake cha pili katika klabu hiyo baada ya kutumia kipindi cha pili cha kampeni ya 2022-23 kwa mkopo Stamford Bridge.

Lakini Félix ameanza katika mechi tatu tu za Ligi Kuu chini ya kocha Enzo Maresca.

Hakuna chaguo la ununuzi ambalo limejumuishwa katika mpango huo.

Ingawa klabu hiyo haijafichua undani wa makubaliano hayo na Chelsea, inaripotiwa Milan italipa ada ya mkopo ya euro milioni 2 hadi 3.

Klabu hiyo ya Serie A pia itakuwa inamlipa mshahara wake wote.

Félix, ambaye ana mkataba na The Blues hadi Juni 2031, anakuwa mchezaji wa tano kusajiliwa na Milan katika dirisha la Januari.

The Rossoneri walitawala dirisha la Italia baada ya kumleta beki wa England, Kyle Walker kutoka Manchester City na mshambuliaji wa Mexico, Santiago Giménez kutoka Feyenoord.

Kiungo Warren Bondo pia alijiunga na AC Milan kwa uhamisho wa kudumu kutoka Monza huku mshambuliaji Riccardo Sottil akijiunga kwa mkopo kutoka Fiorentina huku chaguo la kumnunua likijumuishwa katika mkataba huo.

# City kinara matumizi usajili Januari

**LONDON,** England

KLABU za Ligi Kuu England, zilitumia takriban pauni milioni 370 katika dirisha la usajili la majira ya baridi la Januari, huku Manchester City ikitumia pauni milioni 180, karibu sawa na timu nyingine 19.

Kwa mujibu wa BBC Sport, matumizi ya City yamekuwa ya pili kuwa juu zaidi katika dirisha la majira ya baridi, huku rekodi ya Chelsea ikiwa bado ni pauni milioni 275 mwaka 2023.

Matumizi yameongezeka kwa pauni milioni 100 ambayo klabu za Ligi Kuu England zilitoa mwaka mmoja uliopita, lakini ni mbali na rekodi ya pauni milioni 815 iliyowekwa mwaka 2023.

Kikosi cha Pep Guardiola kimemleta Omar Marmoush kutoka Eintracht Frankfurt kwa uhamisho wa pauni milioni 59, akifuatiwa na Vitor Reis wa Palmeiras kwa pauni milioni 29.6 na Abdukodir Khusanov kutoka Lens kwa pauni milioni 33.6.

Kabla ya tarehe ya mwisho, City walimsajili Nico González wa FC Porto kwa kutumia pauni milioni 50.

Tofauti na Ligi Kuu England lilikuwa ni dirisha tulivu kwa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, huku kukiwa na euro milioni 25.13 pekee zilizotumika, kwa mujibu wa Transfermarkt.

Real Betis walifanya usajili mkubwa zaidi kwenye LaLiga siku ya mwisho kwa kumnunua mshambuliaji wa Colombia "Cucho" Hernández kutoka Columbus Crew ya Ligi Kuu ya Marekani, MLS, kwa uhamisho wa euro milioni 13.

Real Madrid, Barcelona na Atlético Madrid walikuwa miongoni mwa klabu za Hispania ambazo hazikuleta uimarishaji wowote katika dirisha hili.



# Kasongo: Ushindani mzunguko wa 2 safi

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Bodi ya Ligi Kuu Nchini (TPLB), imesema imeridhishwa na ushindani unaoonyeshwa katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyoanza kwenye mzunguko wa pili hivi karibuni, imeahidi kufuatilia kwa karibu zaidi michezo yote ili kuhakikisha inachezwa kwa kufuata sheria na kanuni za soka.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi, Almasi Kasongo, alisema ushindani huo 'unasadifu' kile kilichotangazwa hivi karibuni na Shirikisho la Kimataifa la Historia na Takwimu za Mpira wa Miguu (IFFHS), kuwa ligi hiyo inashika nafasi ya nne kwa ubora Afrika.

"Ligi Kuu imekuwa na ushindani mkubwa, tunaridhishwa na kila kitu kinachoendelea, kwa hiyo sisi kama wasimamizi tumejipanga kuendana na kasi ya ushindani.

Ni imani yetu tutaendelea kusimamia kwa weledi, uwazi, yaani tutakuwa karibu zaidi na michezo yote iliyobaki ili kuhakikisha inachezwa kwa kanuni tulizokuwa nazo na kuzingatia sheria 17 za soka," alisema Kasongo.

Aliongeza changamoto waliyonayo kama wasimamizi ni kuendelea kuilinda nafasi hiyo, pamoja na kuelekea kupanda hadhi ambako wanakuhitaji na ili kufika huko anafahamu kazi ya ziada inatakiwa kufanyika.

"uzi hapa Ligi yetu imetangazwa ni ya nne kwa ubora barani Afrika, unaweza kuona kuna kazi kubwa inafanyika kutoka kwa wadhamini, klabu zenyewe, wanahabari na sisi wasimamizi.

Hivi karibuni kumekuwa na maoni na mawazo mbalimbali huku wengine wakidai Ligi Kuu Tanzania Bara ni dhaifu na imekuwa ikisababisha baadhi ya timu kukosa ushindani katika michezo ya kimataifa.

Aliyekuwa Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, hivi karibuni alitoa maoni yake kuhusu hilo, baada ya timu yake kutolewa katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ikishindwa kutinga hatua ya robo fainali, lakini baadhi wakapinga kwa sababu Simba ipo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara inayotajwa ni dhaifu, lakini imesonga mbele.

Simba ndio wawakilishi pekee wa Afrika Mashariki na Kati waliobakia katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

# TAOUSSI AIKARIBISHA KMC AKIIPIGIA HESABU SIMBA

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI inatarajia kuwakaribisha KMC FC katika mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, tayari Azam imeanza mikakati ya kuhakikisha inapata ushindi dhidi ya Simba.

**Wekundu wa Msimbazi atakuwa mwenyeji wa mechi hiyo itakayochezwa Februari 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.**

Mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Septemba 26, mwaka jana wenyeji Azam walikubali kichapo cha mabao 2-0.

Akizungumza jijini jana, Kocha Mkuu wa Azam FC, Rachid Taoussi, alisema kwa sasa akili zao ni mchezo wa leo usiku dhidi ya KMC lakini amekiri anaufikiria pia mchezo dhidi ya Simba.

"Hatuwezi kuacha kuufikiria mchezo dhidi ya Simba, ni mchezo mkubwa, tulipoteza katika mchezo wa kwanza, tuna nafasi ya kulipiza kisasi, hatutakubali kuona tunapoteza mchezo wa pili kwa Simba, lakini kwa sasa akili zetu zipo kwenye michezo iliyopo mbele kabla ya mchezo huo," alisema Taoussi.

Naye kiungo wa timu hiyo, Feisal Salum 'Fei Toto' amesema mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zinazidi kuwa na ushindani kwa sababu wameingia hatua ya lala salama.

Fei Toto, alisema wakati huu kila timu inashuka uwanjani ikiwa na malengo yake na hivyo hakuna mchezo rahisi au mwepesi.

"Hakuna mechi inayotabirika, ni muda wa mapambano kwa kila timu, sisi kwetu wachezaji tumejipanga vizuri kuhakikisha tunashinda kila mechi," alisema kiungo huyo kutoka Zanzibar.

Kwa mujibu wa ratiba ya Ligi Kuu, Yanga watacheza michezo minne kabla ya kukutana na watani zao Simba, wataanza leo dhidi ya KMC, kabla ya Jumapili ijayo kuwakaribisha Pamba Jiji kutoka jijini, Mwanza.

Baada ya hapo Azam watawakaribisha Mashujaa FC ya Kigoma mechi itakayochezwa Februari 15, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex kabla ya kuifuata Coastal Union siku nne baadaye halafu ikitarajiwa kurejea Dar es Salaam kuisubiri Simba.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara huku vinara wa ligi hiyo ni Simba yenye pointi 43.



Mkurugenzi wa Ufundi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Oscar Mirambo (katikati), akitoa maelekezo kwa wachezaji chipukizi wenye umri chini ya miaka 17 wanaolelewa katika Kituo cha Programu za vijana cha TDS kilichopo kwenye Uwanja wa Mnyanjani jijini, Tanga. **PICHA: TFF**

# *Mtibwa: Tutarejea Ligi Kuu mapema*

**Na Somoe Ng'itu**

UONGOZI wa Mtibwa Sugar unatamba timu yao itarejea mapema katika Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na mechi nyingi 'mkononi'.

Mtibwa Sugar yenye pointi 44 ndio vinara wa Ligi ya Championship inayoendelea katika viwanja mbalimbali nchini. Thobias Kifaru, Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, aliliambia Nipashe, wana kikosi imara na kilichojipanga vyema kuhakikisha wanatimiza mipango yao ya kurejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kifaru alisema wachezaji, benchi la ufundi na viongozi wa timu hiyo wanafahamu walipokosea na sasa wamejiimarisha katika kila idara ili kupata matokeo chanya.

"Tunajivunia ubora wa kikosi chetu, tuna wachezaji wenye uwezo na wanaofahamu malengo ya klabu, sisi tutarejea Ligi Kuu Tanzania Bara mapema sana, tayari tumeshaona hesabu zetu zinatuambia," Kifaru alitamba.

Aliongeza mbali na kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara, pia wanahitaji kutwaa Tuzo ya Mfungaji Bora wa Ligi ya Championship kwa msimu huu.

"Mshambuliaji wetu Raizin (Khalfan), amekuwa chachu katika kufikia malengo, ataendelea kutikisa nyavu za wapinzani katika kila mechi, tumecheza michezo 17 na yeye amefunga mabao 14, hii inaonyesha yuko vizuri," aliongeza Kifaru.

Nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo inashikiliwa na Geita Gold yenye pointi 36 ikifuatiwa na Mbeya City na Stand United zenye pointi 35 kila moja.

# Michezo

Alhamisi Februari 6, 2025
Nipashe



City kinara matumizi usajili Januari UKURASA 22



Kiungo mshambuliaji wa kimataifa wa Yanga, Stephanie Aziz Ki (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa KenGold kutoka Mbeya katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana. Yanga ilishinda mabao 6-1. **PICHA: YANGA SC**

## Mo: Kibu hauzwi, Simba SC ikiwaandalia dozi Fountain

**Na Adam Fungamwango**

IKITARAJIWA kuwakabili wenyeji Fountain Gate FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa ulioko Babati mkoani Manyara, Wekundu wa Msimbazi wamekataa kumuuza nyota wao, Denis Kibu, kwa MC Algers ya Algeria, imefahamika.

Mechi ya leo itakuwa ni mchezo wa tisa kwa Simba kushuka nje ya uwanja wake wa nyumbani, ambapo katika michezo nane imepata ushindi wa asilimia 100.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, aliliambia gazeti hili, timu yake imejipanga kuondoka na pointi tatu muhimu ili kuendeleza kutoa dozi katika kila inapocheza ugenini msimu huu.

Kocha huyo alisema Simba imekuwa na matokeo mazuri inapocheza ugenini na hii inachagizwa na idadi kubwa ya mashabiki wanaojitokeza viwanjani kuwashangilia wachezaji wao.

Hata hivyo, Simba inaweza kumkosa winga wake tegemeo, Kibu, aliyeumia katika mchezo uliopita, ingawa daktari wa timu, Edwin Kagoba, amesema hali yake inaendelea vizuri.

"Yuko katika hatua ya pili ya matibabu, tunategemea, atakapopita kwenye hatua zote za matibabu anaweza kuwapo kwenye mchezo wetu ujao. Ila hii uwepo wake ni nusu kwa nusu, kuna vitu tunaviangalia leo (jana) na kesho (leo), lakini niwatoe hofu wanachama na mashabiki wa Simba hali yake si mbaya si ya kumweka nje muda mrefu," alisema daktari huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Fountain Gate, raia wa Kenya, Robert Matano, amesema amekiandaa vyema kikosi chake kushindana na Simba, ingawa anaamini watawapa upinzani mkali.

"Ninataka kushinda, najua utakuwa mchezo wa kwanza kwangu tangu niichukue timu, hapa siwezi kueleza sana siri zangu za vita, subirini dakika 90," alisema Matano.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Mohamed Dewji 'Mo', amesema klabu hiyo haiko tayari kumuuza Kibu kwa sababu inapambana kuwania taji la Ligi Kuu na inahitaji kufanya vyema katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# Yanga yamkaribisha Hamdi kibabe

**Na Faustine Feliciane**

## ●●● Kocha huyo amrithi Ramovic, Diarra atunguliwa wakiisulubu KenGold...

MABINGWA watetezi, Yanga wamemkaribisha Kocha Mkuu mpya, Miloud Hamdi, kwa kupata ushindi mnono wa mabao 6-1 dhidi ya KenGold katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana.

**Hamdi ametua Yanga akitokea Singida Black Stars ya mkoani Singida, akiwa amerithi mikoba iliyoachwa na Sead Ramovic, aliyeachana na klabu hiyo ya Jangwani baada ya kufanikiwa kupata dau nono kutoka kwa CR Belouizdad ya Algeria.**

Kocha huyo mpya wa Yanga jana alikuwa jukwaani akishuhudia timu yake mpya ikipata ushindi mnono dhidi ya KenGold inayoburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini akiandika 'dondo' ambazo huenda akazitumia katika majukumu yake mapya.

Yanga ilitoa taarifa ya kuachana na Ramovic kwa kueleza walifikia makubaliano ya pande mbili ya kuvunja mkataba.

Katika mchezo wa jana, Yanga walianza kwa kasi na iliwachukua dakika moja tu kuandika bao la kwanza kupitia kwa Prince Dube aliyepokea pasi safi ndani ya eneo la hatari kutoka kwa Stephanie Aziz Ki.

Kupatikana kwa bao hilo ni kama kuliwavuruga wachezaji wa KenGold ambao walipoteza utulivu na kuipa nafasi Yanga kufanya mashambulizi yaliyozalisha bao la pili lililofungwa na Clement Mzize ambaye jana alifikisha magoli tisa.

Kengold licha ya kufanya maboresho ya timu yake katika dirisha dogo la usajili walishindwa kabisa kuhimili kasi ya Yanga huku Pacome Zouazoua akiipatia timu yake bao la tatu dakika ya 38 akiunganisha vizuri pasi ya Mzize.

Mpaka mwamuzi anapuliza filimbi ya kumalizika kipindi cha kwanza, Yanga ilikuwa mbele kwa mabao 4-0.

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi na Yanga kama ilivyokuwa kipindi cha kwanza, iliwachukua tena dakika moja mabingwa hao watetezi kuandika bao la tano kupitia kwa Dube na kama straika huyo Mzimbabwe angeweka makini angefunga 'hat trick' kama angetumia vizuri pasi safi ya mtokea benchi, Clatous Chama, alipiga pembeni.

Dakika ya 84, Duke Abuya, aliipatia Yanga bao la sita akiunganisha kwa shuti mpira uliotoka kwa Keneth Musonda, ambaye wote waliingia kipindi cha pili kuchukua nafasi za Mudathir Yahaya na Pacome.

Mshambuliaji wa Kengold, Selemani Rashid, alimshangaza kipa wa Yanga, Djigui Diarra, baada ya kupiga mpira mrefu katikati ya uwanja eneo la kuanzisha mpira na kutinga wavuni baada ya kushindwa kuokoa hatari hiyo na kufuta 'clean sheet' ambayo angeweza kuondoka nayo.

Matokeo hayo yanaifanya Yanga kupanda kileleni mwa msimamo wakifikisha pointi 45 baada ya kucheza michezo 17 lakini wanaweza kushushwa endapo Simba inayoshuka ugenini dhidi ya Fountain Gate itapata ushindi wowote.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002